JACKPOT BABA LAO!
TZS. 472,189,430
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



## Wadau wasifu ongezeko 'boom' vyuoni, watoa hoja ya hadhari

UKURASA 2




UKURASA 11

# Nipashe

Jumatatu Februari 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581220

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



RIPOTI MAALUM

# Mabinti washawishiwa kufanya ngono wapate bahati ya kuolewa

• **Uchunguzi** vijijini wabaini wanaomsindikiza dada wananasa kwenye mitego ya shemeji zao... *Endelea Uk. 4*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akizungumza na Suleiman Ali Abdalla, mfanyabiashara wa duka la chakula na bidhaa mbalimbali kujua bei za chakula alipotembelea Soko Kuu la Chakechake wilayani Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba jana. **PICHA: IKULU**

## Mpangaji adaiwa kumuua mwenye nyumba kisa deni

UKURASA 2

REACH A WIDER AUDIENCE THIS Valentine SEASON
AT AN AMAZING OFFER
UP TO 25% Off
On valentine season advertisements*
FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023
The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY
Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY
TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area
Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com
*Terms and conditions apply.
Followus: @Theguardiantz



## Mgodi matatani kutiririsha sumu kwenye vyanzo vya maji

UKURASA 16

# Mpangaji adaiwa kumuua mwenye nyumba kisa deni

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKULIMA wa Kijiji na Kata ya Likongowele, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Siamini Mtopoka (40), anadaiwa kuuawa na mpangaji wake Shabani Matola kwa kukatwa na panga kichwani kwa kile kilichodaiwa ugomvi wa malipo ya kodi.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka eneo hilo zilizothibitishwa na uongozi wa kata husika na mamlaka ya kulinda usalama wa raia na mali zao mkoani Lindi, tukio hilo lilitokea Februari 5, mwaka huu.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, wakiwamo Mussa Daudi, Hemedi Kindamba, Somoe Isumaili na Ashura Ally, walidai chanzo cha tukio hilo ni baba mwenye nyumba kufika alikokuwa anaishi mpangaji huyo kumdai malipo ya pango la nyumba. Walidai kuwa madai ya mmiliki huyo yalipingwa na mpangaji wake baada ya kumweleza kuwa kama anahitaji pango la nyumba yake, amlipe kwanza fedha alizokuwa anamdai kutokana na kazi aliyokuwa amempa ya kubangua korosho.

Mashuhuda hao walidai kauli iliyotolewa na mpangaji huyo haikumfurahisha mwenye nyumba ambaye alifunga mlango kwa nje na kuelekea Ofisi ya Ofisa Mtendaji Kata kwa lengo la kumshtaki mpangaji wake.

Walidai kuwa wakati akiwa njiani, mpangaji alivunja mlango, akatoka na kumfuata mwenye nyumba akiwa na panga mkononi na alipompata njiani, alimpiga panga la kichwani akaanguka chini akafariki dunia papohapo.

Walidai kuwa watu walipooona tukio hilo, walimkamata mpangaji huyo na kumkabidhi kwenye Kituo cha Polisi cha mjini Liwale.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Likongowele, Augustino Mbogo alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa mtuhumiwa yuko polisi kwa hatua za kisheria.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Pili Mande, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mtuhumiwa Shaban Matola amekamatwa na upelelezi ukikamilika, atafikishwa mahakamani.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya China Harbour Engineering wakiendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa gati kwenye Bandari ya Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania, Iran kuendeleza ushirikiano wa nyanja zote

**Na James Kandoya**

TANZANIA na Iran zimekubaliana kuendeleza ushirikiano kwenye nyanja za uchumi, biashara na uwekezaji kwa maslahi ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki , Dk. Stergomena Tax, alisema hayo kwenye maadhimisho ya miaka 44 ya mapinduzi ya Iran na miaka 40 ya ushirikiano wa kidiplomasia na Tanzania yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Alisema nchi hizo mbili zimeshirikiana katika njanja mbalimbali ikiwamo za afya, elimu, utamaduni na kilimo.

Alisema Tanzania itaendelea kushirikiana kwa karibu na Jamhuri ya Kiislam ya Iran kuleta maendeleo kwa maslahi mapana ya watu wa nchi mbili.

Waziri Tax alipongeza Iran kwa kasi ya maendeleo katika nyanja za kiuchumi na kijamii katika kipindi chote cha miaka 44 ya mapinduzi.

Balozi wa Iran nchini, Hossein Alvandi Bahineh, alisema biashara kati ya nchi hizo mbili imekua kutoka dola za kimarekani milioni 20 hadi kufikia milioni 70 mwaka uliopita.

Balozi huyo alisema katika kipindi cha miaka 40, nchi hizo zimeshirikiana kimataifa katika njanja za kisiasa, uchumi na utamaduni.

"Jamhuri ya Iran iko tayari kuendeleza ushirikiano na Tanzania katika nyanja za uchumi, siasa na utamaduni kwa maslahi ya wananchi wetu wa nchi mbili," alisema balozi huyo.

Aliongeza kuwa nchi ya Iran iko tayari kusaidia maendeleo ya Tanzania.

# Wadau wapongeza uamuzi kuongeza 'boom' vyuoni

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa elimu, wanaharakati na wanasiasa wametoa maoni yao kuhusu ongezeko la fedha ya kujikimu kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Sh. 8,500 ya sasa hadi Sh. 10,000 kwa siku.

Maoni ya wadau hao kwa Nipashe jana, yamekuja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kusudio hilo juzi kwenye mkutano wake na wanafunzi na viongozi wa Jumuiya ya Vyuo Vikuu (TAHLISO) pamoja na ZAHLIFE ya Zanzibar.

Mwanaharakati Hellen Kijo-Bisimba, akitoa maoni kuhusu uamuzi huo wa Rais, alisema ni hatua ya kupongezwa ingawa utaratibu wa namna ya kila mwanafunzi kupata mikopo unapaswa kuwa wa haki na usawa.

"Tunashukuru kwa hatua hiyo, ila namna ya kupata fedha hizo kuna malalamiko mengi kwa sababu fedha hiyo ni ya mkopo na sio ya bure, italipwa, basi mwenye uhitaji apatiwe. Utakuta wanaostahili kupata asilimia 100 anapata asilimia 40, mwenye kupata asilimia 40 anapata 100.

"Itolewe kwa haki ili kila mnufaika aweze kupata. Kuna malalamiko namna ya kupata, nina ushahidi kabisa utakuta mtoto ni yatima, hana baba wala mama, anakosa mkopo au mtoto ambaye amesoma shule binafsi hapewi, utakuta elimu hiyo alisoma kwa msaada wa kulipiwa," alisema Kijo-BIsimba ambaye aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii kilichoko Kipunguni, Dar es Salaam, Selemani Bishagazi, alisema ongezeko la fedha ya kujikimu wanafunzi wa elimu ya juu, linapaswa liendane na vyanzo vilivyoko kuwa imara na kuanzishwa vipya vya ukusanyaji mapato.

Alisema kuongezwa wanafunzi fedha hiyo, isiongeze ugumu wa maisha kwa upande mwingine, yaani tozo na kwamba hivi sasa serikali iboreshe mifumo ya ukusanyaji mapato ambayo husababisha kutokusanywa fedha ipasavyo.

"Kungekuwa na mifumo ya kudhibiti kwanza fedha, mapato, lakini hiyo pesa inatoka wapi? Hatuoni vyanzo vipya. Tuanzishe vyanzo vya mapato vipya au tulivyonavyo viwe thabiti, vikusanye kwa usahihi. Mfano EFD mashine zinatakiwa zitolewe bure, ili kila mfanyabiashara alipe mapato.

"Vyanzo vingi vya mapato havijafikiwa au vinavuja, kwa mfano utakuta mtu anapaki gari lake popote pale iliyojaa maziwa, anauza maziwa gari zima, bila hata risiti, anamaliza anaondoka, Kariakoo biashara nyingi hazina risiti," alisema mwanaharakati huyo.

Pia alisema serikali inapaswa ishughulikie changamoto zingine vyuoni, zikiwamo rushwa hasa ya ngono, akisema utafiti ulikwishabaini tatizo hilo, na linawaathiri zaidi wanawake na kuondoa utu wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, alisema wakati serikali ikitamka kuongeza fedha hiyo, wanafunzi nao waitumie fedha kwa malengo husika.

"Utakuta mtu anakwenda chuoni tayari ana nguo za kuvaa, lakini akifika huko anaanza tamaa ananunua nguo za kumlinda kimazingira, yaani aendane na mazingira, badala ya fedha aliyopewa kumsaidia kitaaluma, kula," alisema Janeth na kuongeza:

"Fedha hizi zilizoongezwa zitamsaidia mtoto anayetoka kwenye kaya duni, kwa sababu huko kwenye kijiji hadi vikao vinakaa kijijini, hii angalau itasaidia hasa wazazi kupunguziwa mzigo, walijikuta wanafanya kazi ngumu kuhakikisha mtoto asome."

Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana Chama cha ACT-Wazalendo, Abdul Nondo alisema ongezeko la fedha hiyo limekuja kipindi mwafaka ambao hivi sasa, gharama za maisha zimekuwa juu.

Juzi Rais Samia, alipokuwa anatangaza neema hiyo vyuoni, alisema: "Suala la 'boom' (posho ya kujikimu), boom likimalizika mnapiga pasi ndefu, unakula mara moja kwa siku, Waziri wa Elimu, nenda kaangalie, tutaanza na Sh. 10,000."

Rais alisema kwamba vijana wenye sifa ya kuingia vyuoni na wazazi wao hawana uwezo, serikali imezungumza na benki ya NMB iliyotenga Sh. bilioni 200 kwa ajili yao, kwa ajili ya kutoa mikopo ya riba nafuu.

Alibainisha kuwa hatua nyingine inayochukuliwa na serikali ni kuzungumza na baadhi ya mataifa kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Alisema wakati nchi inapata uhuru, chuo kikuu kilikuwa kimoja na sasa kuna vyuo vikuu 30 na kati ya hivyo 12 ni vya serikali na binafsi 18.

Wakati Rais Samia alipoingia madarakani, Machi mwaka 2021, mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu iliyokuwa inatolewa ni Sh. bilioni 464 kwa mwaka na sasa imefikia Sh. bilioni 654.

**TANGAZO**

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

**1. POSITION: CABIN CREW II (90 POSTS)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Must havea minimum of Form IV Certificate with Four Credit passes of which ONE of them should be English and;
- Must hold Ab-Initio Certificate from Recognized Aviation Institution plus Cabin Crew License from Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA);
- Must be Fluent in both written and spoken English and Swahili
- Must have no visible tattoos while in Air Tanzania crew uniform
- Minimum height of 160cm
- Arm reach of 212cm while standing
- Physically fit for this demanding role with a healthy Body Mass Index
- Knowledge of Extra International Language will be an added advantage

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Ensure passenger's safety and security from the time passengers aboard the aircraft until the time they disembark.
- Inform passengers on emergency, safety and security procedures during all phases of the flight.
- Ensure cabin safety and security under the overall authority and responsibility of the PIC (i.e the safety of passengers and security of cabin load and galleys)
- Responsible to read and sign all notices or bulletins as required.
- Attend preflight and post flight briefing as required
- Ensure to carry out a cabin security check, verify the safety emergency equipment, aircraft system, catering equipment's and immediately report any deficiencies to the Flight Purser/ In charge cabin crew for further action.
- Ensure passengers respect and comply with the "fasten seatbelt" and "No smoking "signs and other safety and security instructions while in flight.
- Ensure the passengers safely escape in an emergency evacuation.
- Form the liaison between passengers and the flight crew
- Provide optimum comfort and service to the customers.
- Report to the Senior Cabin Crew and Flight Purser any incident that has endangered or may endangered safety of the operations while on flying duties the Cabin crew is required to follow all lawful directions given by the Senior Cabin Crew/Flight Purser (in charge cabin crew)
- Ensures the safety and security of passengers, crew and aircraft through adherence to Company policies and standard operating procedures.
- Deliver world class passenger service and assist in on-time performance

**2. POSITION: FLIGHT OPERATIONS ASSISTANT II (7 POSTS)**

**2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Holder of Advanced Level Certificate of Secondary Education preferable in Science subject or equivalent.
- Must have a Certificate of Flight Operations/ Flight Dispatch or Equivalent
- Must be a holder of TCAA Flight Operations/Flight Dispatcher's License
- Must be proficient in English Language in accordance with the English Language proficiency requirement contained in TCAR.
- Must be computer literate.

**2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Monitoring crew reporting on/off duty and crew duty time limitations
- Checking contents of operational documents and ensure that all flights have the right documents
- Assisting in preparation of the ATS flight plan
- Assisting in compiling NOTAM and Meteorological report folders for flight
- Obtaining aircraft defect report from line maintenance
- Assisting in preparation of operational forms and voyage report forms
- Supporting, briefing and/or assisting the FOO
- In the absence of FOO briefing and/or assisting the PIC
- Makes recommendation in areas of expertise
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**3. POSITION: SENIOR PILOT I (CAPTAIN) - (17 POSTS)**

**3.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons equipment or above with a good performance.
- Must hold a valid TCAA Medical Certificate.
- Must have successfully completed the appropriate Flight Training Courses according Operations Manual Part D and Manufacturer training manuals.

**3.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
- Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
- Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
- Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
- Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
- Report all incidents and accidents.
- Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
- Report any Flight delays of flights.
- Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**4. POSITION: PILOT II (FIRST OFFICER) - (17 POSTS)**

**4.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have flown with more than 250 flying hours or above with Commercial Pilot License, Multi Engine with Instrument Rating.
- Must hold a valid TCAA Medical Certificate.
- Must have successfully completed the appropriate Flight Training Courses according Operations Manual Part D and Manufacturer training manuals.

**4.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- To participate in the Pilot-in-Command's crew briefing, and make himself aware of all relevant aeronautical and meteorological information as well as relevant papers documenting the aircraft technical status and its anticipated load.
- To prepare the OFP and when necessary, file the ATS Flight Plan with the appropriate Authority. If stored plans are used then he should ensure that the correct plan has been activated
- To carry out such duties concerning the flight in accordance with the SOP, including procedures, limitations and performance related to the specific aircraft type, as allocated to him by the Pilot-in-Command;
- To confirm the safe navigation of the aircraft, maintaining a continuous and independent check upon both the geographical position of the aircraft and its safe terrain clearance
- To safely and properly conduct the flight in compliance with the current flight plan and the Pilot-in-Command's instructions when the Pilot-in-Command is not at the controls. Any change to the current flight plan has to be notified to the Pilot-in Command.
- To provide advice, information and assistance to the Pilot-in-Command, as may contribute favorable towards the safe and efficient conduct of the flight.
- To assist the Pilot-in-Command in administration duties related to the flight and
- To seek and receive information and/or explanation from the Pilot-in Command, as may be necessary to enable fulfilment of functions.
- To assist the Flight Safety Department for all Technical related matters
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**5. POSITION: PROCUREMENT OFFICER II (4 POSTS)**

**5.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Procurement and Supplies Management, Material Management, Stores Management, Logistics Management.
- Must be registered by PSPTB as Graduate Procurement and Supplies Professional.

**5.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- To prepare bid documents and Tender advertisements
- To prepare contract documents or purchases orders to approved bidders
- To seek approval to purchase the identified requirements
- To Participate in preparation of Annual Procurement Plan (APP)
- To participate in preparation of monthly, quarterly and annual procurement reports
- To receive, verifying, and submitting invoice of delivered goods or completed service for payment
- Participate in preparation for stock taking
- Liaise with suppliers for timely delivery of the goods
- To Maintain store records
- To receive and issue goods to user department, processing stores requisitions, order expedition, inventory and stock replenishment
- To perform any other related duties as may be assigned by the supervisor

**6. TERMS AND CONDITIONS:**

Five (5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**7. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. A full size picture dressed in business attire for Cabin Crew
v. Name and address of at least two reputable referees;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**8. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on 13th February, 2023**

***ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.***

RIPOTI MAALUM

# Mabinti washawishiwa kufanya ngono wapate bahati kuolewa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

## - Wanaomsindikiza dada wananasa mitego ya shemeji
## -Ni kupitia ndoa za Bukwilima za kabila la Wasukuma



NDOA za kimila za kabila la Wasukuma zinazofahamika kama Bukwilima ambazo zimekuwa zikifanyika maeneo mbalimbali ya vijijini mkoani Shinyanga, zimetajwa kuwa kichocheo cha kuendelea kuwapo kwa ndoa za utotoni kwenye eneo hilo la Kanda ya Ziwa.

Bukwilima ni ndoa ambazo zinatajwa kuwaweka mabinti kwenye mazingira hatari ya kushawishiwa kufanya ngono na wanaume (hata katika umri mdogo) ili wapate bahati ya kuolewa.

John Myola, Mkurugenzi wa Shirika la Agape linalojihusisha na utetezi wa haki za watoto mkoani Shinyanga, anasema: "Neno 'Bukwilima' maana yake ni bwana harusi kusindikizwa na wanaume wenzake pale anapokuwa anakwenda kuoa.

"Kwa hiyo husindikizwa kwenda ukweni, yaani nyumbani kwa mwanamke kwa ajili ya kuoa ambako hukaa kwa siku mbili hadi tatu wakisubiri siku ya harusi," anasema Myola.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa katika siku hizo, wanaume waliomsindikiza huandaliwa mabinti ambao hawajaolewa ambao huwahudumia kama waume zao (Bakwilima) kwa lengo la kutimiza kinachoitwa 'kuwafariji'.

Myola ambaye shirika lake la Agape pia linajihusisha na kusomesha watoto manusura wa ndoa za utotoni, anaeleza kuwa ndoa hizo za kimila ni kikwazo cha jitihada za kukomesha ndoa za utotoni.

Kijijini Ilobashi, Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, ni miongoni mwa maeneo yanayotajwa kukabiliwa na ndoa za kimila. Mwelimishaji masuala ya ukatili ndani ya jamii kwenye kijiji hicho, Mary Lutinya anasema msimu wa mavuno kijijini humo hufanyika ndoa nyingi za kimila, ambazo anazitaja ni chanzo cha ndoa za utotoni.

Kwa mujibu wa takwimu za Utafiti wa Idadi ya watu na Afya (TDHS) ya Mwaka 2015/16, mwanamke mmoja kati ya watatu nchini huolewa kabla ya kutimiza miaka 18. Utafiti huo pia unaonyesha kuwapo ongezeko la asilimia tano la ndoa za wasichana walio katika rika balehe (umri wa miaka 15-19) tangu utafiti wa awali mwaka 2010.

**USHUHUDA KIJIJINI**

Mmoja wa wanawake aliyewahi kushiriki kwenye ndoa ya aina hiyo ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga (jina tunalihifadhiwa), anasimulia kuwa wanapokuwa ndani ya nyumba na wanaume hao, hula pamoja na kila mwanamume huketi karibu na binti mithili ya wapenzi na kuna wakati hutakiwa kulishana chakula, utaratibu huo umepewa jina la 'yakodelemela shemeji' (yaani pokea tonge shemeji).

Anasema mazungumzo yao mengi huwa yanahusu mapenzi na kurubuniana kwamba wataoana na ikifika muda wa usiku baadhi yao hutumbukia kwenye kufanya mapenzi lakini hapo ni sharti kuwe na rukhsa ya binti kwenda nje ya nyumba wanamolala mabinti inayotolewa na mkuu wao.

"Huwa tunatengewa nyumba moja kwa ajili ya kulala mabinti na moja kwa ajili ya wale wanaume. Hiyo nyumba ya wanaume ndiyo inayotumika kuwapelekea chakula na ndimo tunakula kwa pamoja nao.

"Kimsingi, ambayo hufanyika ndani ya chumba hicho ni uchafu ambao siyo rahisi kuamini, lakini kutokana na kutojitambua kipindi hicho pamoja na kulazimishwa na wazazi ili tutimiza mila, tulikuwa tunafanya tu hata japo mimi siziafiki ndoa hizo," anasimulia.

Mwanamke huyo anasema hivi sasa yeye ameolewa na mwanaume tofauti na yule aliyeshiriki naye ngono kwenye ndoa ya Bukwilima, kipindi hicho akiwa mkazi wa Kijiji cha Irobashi kilichoko jirani na Kijiji cha Masengwa anakoishi kwa sasa.

"Baada ya ile ndoa niliendelea na uhusiano na yule mwanamume kama miezi sita hivi, lakini baadaye nilikuja kupata taarifa kwamba tayari alikuwa ameoa mwanamke mwingine na nilipofuatilia nilibaini ni kweli. Hapo na mimi nikaona sina budi kuolewa.

"Kumbuka wale wanaume wanaomsindikiza mwoaji, wanapokuja wanakuwa mchanganyiko wa walioa na ambao bado hawajaoa. Kwa hiyo, binti kudanganywa na kutumbukia kwa mume wa mtu ni rahisi," anahadharisha.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, anabainisha kuwa ndoa ya Bukwilima ikishafungwa, mabinti kutoka kitongoji anakotoka bibi harusi, hutakiwa kwenda ukweni ambako hukaa kwa siku mbili hadi tatu ikiwa ni ishara ya kumsindikiza mwenzao huyo.

Anasema mabinti ambao huchaguliwa ni wale ambao hawajaolewa wakiambatana na wanawake wachache walioolewa pamoja na vijana kutoka kitongoji chao ambao huwabeba mabinti hao, mara nyingi kwa kutumia baiskeli, kila mmoja na wa kwake.

"Huko njiani, kijana aliyembeba binti hutumia muda wote wa safari kumtongoza na kama watakubaliana, watapanga namna ya kufanya mapenzi ndani ya hizo siku mbili au tatu watakazokuwa huko ukweni.

"Kwa mila za huku usukumani, bibi harusi haendi ukweni siku hiyo hiyo ya harusi. Wasindikizaji hutangulia, yeye huwafuata siku ya pili au ya tatu, akishafika, hapo ndipo mabinti wenzake na vijana waliowabeba wanaondoka kurejea nyumbani.

"Mila kama hizi zilishapitwa na wakati. Kwa hiyo, zinapaswa kufutiliwa mbali kabisa maana zinavunja haki za watoto na hazistahili kuwapo katika ulimwengu wa sasa, serikali inapaswa kuliangalia hili, ili kulinda haki za watoto na kutimiza ndoto zao," anawasilisha hoja yake.

Mama wa kimila, Bibi Hamida Ndaki, mkazi wa Kijiji cha Nyamarogo wilayani Shinyanga, anasema anapingana na ndoa za kimila (Bukwilima) kwa sababu zina madhara ambayo huwapata mabinti wanapolala na wanaume, yakijumuisha kupata ujauzito kisha kukataliwa na wahusika, kukatishwa masomo na kubaki nyumbani wakilea watoto wao.

"Wanaume ambao humsindikiza kijana mwoaji huwa ni watu wazima na hukutana na vibinti vidogo vikitafuta bahati ya kuolewa, na wanapofanya mapenzi na watoto hawa, wengine huwapa ujauzito, wakiwaeleza wana ujauzito wao huwakataa na baadhi hukubali," anasema Hamida.

Anasimulia kuwa wanaume hao wanapokuwa na mabinti kwenye mji wa bibi harusi huwa kama wake zao, sababu wanawapatia huduma zote ikiwamo kuwapelekea maji ya kuoga na harusi ya mwenzao ikiisha, wapo wanaobahatika kuolewa na wengine wanaachwa na ujauzito.

Anasema ndoa za namna hiyo kwa sasa zimeshapitwa na wakati kwa sababu haoni maana yoyote ya mabinti kwenda kujitongozesha kwa wanaume wakitafuta bahati ya kuolewa, na wengine kuishia kuharibiwa ndoto zao.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi

**DHANA BUKWILIMA**

Sonda Kabeshi ni mmoja wa wazee wa kimila na mkazi wa Kijiji cha Shatimba wilayani Shinyanga, anasema kwa utamaduni wa kabila la Wasukuma, mtoto akishapevuka anapaswa kuolewa na ndiyo maana wazazi wengi hupenda kuwaozesha mabinti zao ndoa za utotoni.

Kuhusu ndoa za Bukwilima, Kabeshi anasimulia kwamba mabinti wanapokuwa na wanaume hao nyumbani kwa mwanamke anayetarajiwa kuolewa, hupewa nyumba kwa ajili ya maongezi ya pamoja na pia hula pamoja humohumo, mabinti wakiwa watengaji wa chakula hicho kinachoandaliwa na mama zao.

Anasema wakiwa katika nyumba hiyo hufanya maongezi na mabinti ambao wameandaliwa kwa ajili yao.

Anasema wakati wa mazungumzo yao, wakiwa kila mtu na wa kwake, wanaume huwatongoza mabinti hao ili kuwashawishi kufanya nao mapenzi na wengine huahidi kuwaoa.

Manusura wa ndoa za utotoni (jina lake limehifadhiwa) ambaye kwa sasa anaishi Kituo cha Agape, Manispaa ya Shinyanga, ambaye aliozeshwa kwa mahari ya ng'ombe 12 akiwa kidato cha kwanza mwaka 2020, anasema wazazi kuendelea kukumbatia mila za kizamani kunaharibu maisha ya watoto wa kike.

Anasema yeye aliharibiwa ndoto zake za kuja kuwa mwalimu, pale wazazi wake walipoingiwa na tamaa ya kutaka utajiri wa mifugo, wakaamua kumwozesha ndoa ya kimila kwa mwanamume ambaye alikuwa hamfahamu.

"Mimi niliozeshwa na wazazi wangu ndoa ya kimila nikiwa kidato cha kwanza, na siku ninaozeshwa, wazazi wangu hawakuwapo, walikuwa wameshahama Shinyanga kwenda kuishi Morogoro, hivyo ndoa ilibidi ifungwe kwao na mwanamume, lakini maisha ya ndoa yalinishinda nikatoroka na kuja Agape," anasema binti huyo mwenye miaka 18 na kuongeza:

"Ndoa ilinishinda, sikuweza kuvumilia maisha ya kulala na

ITAENDELEA UK. 5

INATOKA UK. 4

# Mabinti washawishiwa kufanya ngono wapate bahati kuolewa

mwanamume kila siku, sababu kila nilipokuwa nikifanya naye tendo la ndoa nilikuwa ninaumia, ndipo nikaona nitoroke kuja Agape na sasa ninaendelea na masomo yangu hapa Shule ya Agape kwa mfumo usio rasmi na mwaka huu ninaingia kidato cha tatu."

Mzazi Ramadhani Kabalo, mkazi wa Shinyanga, anasema wananchi kuendekeza masuala ya mila kandamizi kunachangia ndoa za utotoni mkoani hapa.

Kabalo pia anautaja umaskini umekuwa ukichangia wazazi kuozesha watoto wao ndoa za utotoni ili wapate utajiri wa mifugo.

Mch. Edward Mashala wa Kanisa la P.A.G.T Masengwa wilayani Shinyanga, anasema kuwapo ndoa za kimila ni matokeo ya jamii kupenda kukumbatia mila na desturi zilizopitwa na wakati.

"Wananchi wa maeneo ya vijijini wengi bado wana fikra za kizamani, hivyo wanapaswa kupewa elimu zaidi juu ya madhara ya kuendekeza mila zilizopitwa na wakati na madhara yake ili waishi kisasa," anasema Mch. Mashala.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, Atupokile Maseta, anakiri tatizo la ndoa za kimila lipo kwenye maeneo hayo ya vijijini japo kwa sasa limepungua kwa kiasi kikubwa kulinganishwa na zamani kutokana na elimu ya ukatili ambayo inaendelea kutolewa.

Anasema wao kama viongozi wamekuwa wakilipigia kelele suala hilo pamoja na kutoa elimu ya kujitambua na afya ya uzazi kwa mabinti, wakiwataka kutofanya mapenzi katika umri mdogo, huku wazazi wakielimishwa madhara ya kuozesha watoto.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Aisha Omary, anasema ndoa za kimila ni kikwazo cha vita dhidi ya ndoa za utotoni wilayani humo japo sasa zinapungua kwa kiasi kikubwa.

"Ndoa za utotoni wilayani Shinyanga zimepungua, takwimu za mwaka jana zimefungwa ndoa tatu ambazo tuna taarifa nazo, na zenyewe tulifanikiwa kuzitibua, lakini miaka ya nyuma zilikuwa zikifungwa ndoa hadi 10 kwa mwaka na chanzo cha ndoa hizi ni mila," anasema Aisha.

Anasema mikakati ya serikali wilayani humo ni kuendelea kuelimisha jamii kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari, kuachana na masuala ya kukumbatia mila za kizamnai na kandamizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi hayuko nyuma na kinachoendelea kimila, akisema wana mradi wa kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa jamii ili kuacha vitendo hivyo dhidi ya watoto.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, alipotafutwa na Nipashe wiki iliyopita kuzungumzia suala hilo, alisema tatizo la ndoa za utotoni linasababishwa na wazazi kwa tamaa ya kutaka mali.

"Waandishi wa habari andikeni habari zenye kuonyesha fursa, tangazeni fursa zilizopo ili wazazi wazichangamkie, wapate maendeleo na kuacha kuozesha watoto ndoa za utotoni," alisema Dk. Chaula.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) mwaka 2012, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa ndoa za utotoni kwa asilimia 59 ikifuatiwa na Tabora asilimia 58, na Mara asilimia 55.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA (AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 1 OF 2023

THE REPUBLIC VERSUS

PETER KIPANGULA..........ACCUSED PERSON

To:
Peter Kipangula
Mkenge Magengeni Area, Mkuranga District Council
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 20 day of February 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 20 day of JAN. 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

Served Upon Me/us:
Name..........
Signature..........
Qualification/Relationship
Date..........

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA (AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 11 OF 2023

THE REPUBLIC VERSUS

NANNAH SHOES INTERNATIONAL CO. LIMITED..........ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
Nannah Shoes International Co. Limited
Mwanambaya Village, Mkuranga
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of February 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 2023

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name..........
Signature..........
Qualification/Relationship
Date..........

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA (AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 14 OF 2023

THE REPUBLIC VERSUS

MUHIDIN MOHAMED..........ACCUSED PERSON

To:
Muhidin Mohamed
Mapinga, Bagamoyo District
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of FEBRUARY 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

Served Upon Me/us:
Name..........
Signature..........
Qualification/Relationship
Date..........

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA (AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 5 OF 2023

THE REPUBLIC VERSUS

KIWANGWA PUMP STATION LIMITED..........ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
Kiwangwa Pump Station Limited
Kiwangwa Area, Chalinze
Mwanambaya Village, Mkuranga
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of February 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name..........
Signature..........
Qualification/Relationship
Date..........

---


## KUPOTEA KWA CHETI



**MULHAT MUHDAR HAJI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5249-0007** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ZANZIBAR FEZA SECONDARY SCHOOL mwaka 2017.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/52069/2023**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba, Yanga kwa Mkapa tunataka pointi zote 9 CAF

**BAADA** ya shughuli pevu ugenini kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika mwishoni mwa juma, wiki hii miamba ya soka nchini itakuwa nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mechi zao za raundi ya pili ya hatua ya makundi.

Simba inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi kuikaribisha Raja Casablanca ya Morocco wakati Yanga yenye dhamana hiyo upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Jumapili ikiikaribisha TP Mazembe ya DR Congo uwanjani hapo.

Hata hivyo, Simba imeanza vibaya michuano hiyo kwa kukubali kipigo cha bao 1-0 ugenini nchini Guinea dhidi ya wenyeji wao, Horoya AC, wakati Yanga jana usiku ilikuwa na kibarua kigumu dhidi ya US Monastir nchini Tunisia.

Haijalishi ni matokeo ya aina gani Yanga imeyapata jana usiku, wala yale mabaya iliyoyapata Simba ugenini, kwani katika michuano hii ya Afrika pamoja na kusaka pointi ugenini, hesabu kubwa ni kila timu kuhakikisha inavuna pointi zote tisa za mechi zake za nyumbani na kupigania ushindi ama sare ugenini.

Tayari wapinzani wawili wa Simba, Raja Casablanca na Horoya AC, wameanza vizuri kwa kushinda michezo yao ya awali nyumbani, ambapo miamba hiyo ya Morocco ikiwa kwao ilitoa kipigo kizito cha mabao 5-0 dhidi ya Vipers ya Uganda, hivyo kuongoza Kundi lao la C ikifutiwa na mabingwa hao wa Guinea.

Hivyo, bila kufanya makosa Simba nayo inatakiwa kuhakikisha Jumamosi inaondoka na alama zote tatu dhidi ya Raja Casablanca katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kutinga robo fainali.

Ikumbukwe timu mbili zitakazoshika nafasi ya kwanza na ya pili katika kila kundi, ndizo zitakazotinga hatua ya robo fainali, hivyo kupoteza kwa Simba katika mechi hiyo ya awali ugenini, kunapaswa sasa kufuatiwa na ushindi mkubwa nyumbani dhidi ya Raja Casablanca ambayo inapewa nafasi kubwa ya kuongoza kundi lao.

Tunaamini kwa kaulimbiu ya Simba iliyozoeleka kama "Kwa Mkapa Hatoki Mtu", hakuna kinachoshindikana kama maandalizi makubwa yatafanyika na kila mmoja kuanzia mashabiki, viongozi, benchi la ufundi na muhimu wachezaji, kubeba majukumu yao ipasavyo. Tunataka kuona safari hii Tanzania ikiweka rekodi ya kuingiza timu mbili hatua ya robo fainali, moja Ligi ya Mabingwa na nyingine Kombe la Shirikisho, na hilo litawezekana tu kwanza kwa maandalizi makubwa kuelekea michezo yao ya nyumbani na kisha ile ya ugenini.

Kwa ile ya nyumbani, ni jukumu la kila shabiki, wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla, kujitokeza kwa wingi kuujaza Uwanja wa Mkapa Jumamosi na Jumapili na si kuishia tu kuujaza, bali pia kuende sambamba na kushangilia mwanzo mwisho ili kuwapa hamasa wachezaji wetu.

Tunaamini kama mashabiki na Watanzania kwa ujumla watatumia vema wajibu wao kama mchezaji wa 12 uwanjani kwa kushangilia mwanzo mwisho, hakuna kitakachoshindikana kwa wawakilishi hao wa nchi kubeba pointi zote tisa watakapocheza mechi zao tatu za nyumbani kila mmoja.

Huu ni wakati wa mashabiki wa Simba na Yanga kuweka tofauti na itikadi zao kando na badala yake kuungana na kuwa kitu kimoja katika kuhakikisha wawakilishi hao wa nchi wanasonga mbele.

Nipashe tunaamini, Simba ama Yanga ikishinda Tanzania imeshinda, kwani ushindi wao ni sifa kubwa katika kulitangaza soka letu kimataifa, lakini pia kusonga kwao mbele kutaiwezesha si tu nchi kuingiza timu nne katika michuano hiyo ya CAF msimu ujao, bali pia Ligi Kuu ya Tanzania itazidi kukua na kuvutia wawekezaji wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

## Gonjwa la Simba kwa Horoya AC hili hapa

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Simba, wamepoteza mechi yao ya kwanza kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Horoya ya Guinea.

Watanzania wengi na mashabiki wa soka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati walikuwa wakiifuatilia mechi hiyo iliyochezwa saa 1:00 juzi usiku kwenye ukanda huu na saa 10:00 jioni nchini Guinea, mechi ikipigwa katika Uwanja wa Jenerali Lansana Conte jijini Conakry.

Kwa jinsi nilivyoutazama mchezo huo, niligundua kuwa Simba ilikwenda kwa kuihofia zaidi Horoya kuliko uwezo iliokuwa nao. Inavyoonekana ni kama benchi la Simba halikuisoma vizuri timu hiyo kuliko Horoya iliyowasoma wapinzani wao.

Simba ikaweka viungo wakabaji watatu, Ismael Sawadogo, Sadio Kanoute na Mzamiru Yassin, ikionekana kabisa kuwa mpango mkakati ilikuwa ni kulinda zaidi kuliko kushambulia.

Kama mfumo huu ungekuwa kwa timu za Afrika Kaskazini maarufu kama 'Timu za Waarabu' ambao wao wanaanzia nyuma na kutembeza boli hadi mbele ungeweza kufanya kazi, lakini kilichotokea ni kwamba viungo watatu wa Simba hawakuwa na kazi kubwa sana ya kufanya.

Horoya walikuwa wakipiga mipira mirefu kupeleka mbele kwa washambuliaji na mawinga wao, hawakutaka kabisa kusumbuana na viungo wa Simba katikati ya uwanja.

Na kwa sababu wana wachezaji wengi warefu kuliko hata John Bocco, Sawadogo na Sadio Kanoute, waliwasumbua mno mabeki wa Simba hasa kipindi cha kwanza.

Ukiangalia kwa ujumla ni kwamba Horoya haikuwa timu ya kutisha sana, na kilichoonekana walicheza kwa nidhamu, juhudi, mbinu na kitimu zaidi, lakini hawakuwa na wachezaji wengi wenye vipaji na kutengeneza nafasi kama Simba.

Nadhani kama Simba ingeingia na wazo la kushambulia tangu mwanzo, ingekuwa na mastraika wawili mbele wakati mpira unaanza na ingeua na kiungo mmoja mkabaji, ingeweza kutokana na ushindi kwenye mechi hiyo.

Rejea, kipindi cha pili kuanzia dakika ya 70, ambapo aliingia Bocco, Kibu Denis na Moses Phiri na kubadilisha kabisa mchezo, Horoya wakalazimika kurudi nyuma kuzuia, Simba ikitengeneza nafasi tatu za wazi ambazo wachezaji wake, Bocco na Clatous Chama walishindwa kuzitumia.

Naamini kama benchi la Simba lingekuwa limeisoma Horoya sawa sawa na kugundua wana aina ile ya uchezaji, wala wasingeingia na hofu ya kuwa na viungo watatu wakabaji, badala yake wangeshambulia na kurudi nyuma kuzuia kwa nidhamu.

Walionekana kutoa mianya mingi wanaposhambulia, licha ya kwamba mabeki wao wa kati ni warefu, wana ngumu na wapambanaji.

Hofu hiyo ndiyo iliyosababisha kipindi chote cha kwanza Simba isifanye shambulizi lolote la maana, lakini baada ya benchi la ufundi kuisoma kwa dakika 45 ndipo ilipofahamu inacheza na timu ya aina gani.

Hesabu za wenyeji zilikuwa nzuri, kwani ilionekana wameisoma Simba kuwa hawawezi kushindana nao kati kwa sababu wana wachezaji waliojaliwa vipaji vya kuchezea mpira, hivyo waliwakwepa kwa kupiga mipira ya juu, lengo lao likiwa ni kusaka ushindi tu na si vinginevyo. Pia waliona wachezaji wengi wa Simba ni wafupi dhidi ya wao warefu.

Kingine ni kwamba inaonekana bado wachezaji wa Simba wana matatizo katika kuzuia mipira ya faulo na kona, maarufu kama 'mipira iliyokufa' au ya kutengwa.

Hata bao walilofungwa juzi ni la kona. Mechi ya kirafiki dhidi ya Al Hilal ilikuwa faulo. Mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Yanga, ilikuwa hivyo hivyo. Hata mechi ya ligi hivi karibuni dhidi ya Singida Big Stars ilikuwa faulo pia.

Kwenye mechi ya juzi ilipigwa faulo ya hatari nusura iwe bao, nikamuona Henock Inonga akiwalalamikia wenzake. Huwa kama wamezubaa wanapopigiwa faulo na kona. Wavivu kuruka juu. Na huu ni ugonjwa wa muda mrefu kidogo kwenye kikosi hicho. Ni kama makocha hajapata dawa.

Imefika wakati mashabiki wa Simba wanahofia zaidi faulo na kona kuliko hata penalti. Ukiangalia nao soka kwenye vibanda umiza wanaonekana kuhofia sana wanapopigiwa mpira hiyo. Wanakaa kimya wakisubiri nini kitatokea. Lakini penalti wapo wawili watatu watasema "hiyo Manula anafuta." Na kweli mara nyingi inakuwa hivyo. Ni wajibu sasa kwa benchi la ufundi kuyaangalia hayo na kuyarekebisha ili kufanya vema kwenye mechi zinazofuata.

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yamshikilia mwenyekiti madai ya kujikopesha mil. 94/-

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Singida na Jeshi la Polisi wamemkamata aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Walimu Iramba (CHAMWAI), Ally Mwekwa, kwa madai ya kujikopesha Sh. milioni 94 za chama hicho.

Kukamatwa kwa mwenyekiti huyo kumekuja baada ya kuhojiwa na kukataa saini zilizopo kwenye nyaraka za mtiririko wa fedha zilizokopwa tangu Oktoba 2009 baada ya kuhojiwa.

Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, alitoa agizo kwa vyombo vya usalama kumchukua mwenyekiti huyo wakati akizungumza na walimu zaidi ya 100 juzi ofisini kwake waliofika na kumlalamikia kiongozi wao kwamba hawajalipwa fedha zao zaidi ya Sh. milioni 300 tangu mwaka 2012.

"Wote wanaodaiwa na CHAMWAI hakuna atakayepona, lazima fedha hizo watazirudisha, TAKUKURU na polisi mchukueni huyu mwenyekiti mkafanye uchunguzi wa kitaalamu kuhusu saini kama ni zake au sio zake," aliagiza.

Alisema Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Iramba na Mkalama wapitie upya kuangalia kiwango wanachokatwa watumishi waliokopa fedha katika chama hicho baada ya kubainika baadhi wamekuwa wakikatwa hadi Sh. 2,000 tu kwa mwezi hata kama amechukua mkopo wa Sh. milioni 10.

"Wakurugenzi habari za kuwakata Sh. 2,000 au 4,000 kila mwezi wakati mtu amekopa mamilioni ya fedha haiwezekani na hii ndio inasababisha mikopo kuchukua muda mrefu sana bila kurejeshwa kwenye chama," alisema.


Aliwaagiza viongozi wa Benki ya CRDB kupeleka nyaraka za uthibitisho wa mikopo waliyokuwa wakiwakopesha viongozi wa CHAMWAI, ili kujiridhisha kama taratibu zilifuatwa na kama ikibainika hazikufuatwa, benki hiyo itabeba mzigo wa kulipa fedha za wanachama wanaodai fedha zao.

Serukamba aliwaagiza viongozi wa sasa wa CHAMWAI kupitia upya majina ya watumishi wote wanaodaiwa na wanaokidai chama hicho, ili kuwafahamu na kuweka utaratibu jinsi watakavyozirejesha fedha hizo.

Mwenyekiti mstaafu wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Walimu Iramba (CHAMWAI), Mwekwa, akizungumza na gazeti hili akiwa chini ya ulinzi wa TAKUKURU na polisi, alidai fedha alizokopa ni Sh. milioni 24 na sio milioni 94 kama inavyoelezwa.

"Mimi ninakumbuka nilikopa Sh. milioni 24 kwa nyakati tofauti na nilisharejesha mkopo huo zaidi ya Sh. milioni 25, kwa hilo deni la Sh. milioni 94 silielewi limetoka wapi," alidai.

Inadaiwa baadhi ya viongozi wa chama hicho walijikopesha mamilioni ya shilingi, hali iliyosababisha walimu waliostaafu walipotaka kulipwa fedha zao ikaonekana hakuna fedha zozote kwenye chama.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. ............ OF 20................

THE REPUBLIC
VERSUS

DEUS KIZENGA..................................................................ACCUSED PERSON

To:
Deus Kizenga
Utende Area, Mafia District Council
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 20 day of February 20 23 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 20 day of January 20 23

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

Served Upon Me/us:
Name.........................................
Signature.........................................
Qualification/Relationship
Date.........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 8 OF 20 23

THE REPUBLIC
VERSUS

ELIZABETH HELMAN MTEI..........................................ACCUSED PERSON

To:
Elizabeth Helman Mtei
Picha ya Ndege Area, Kibaha District
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of February 20 23 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 20 23

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

Served Upon Me/us:
Name.........................................
Signature.........................................
Qualification/Relationship
Date.........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 10 OF 20 23

THE REPUBLIC

VERSUS

M.P. MTERENGE.............................................................ACCUSED PERSON

To:
M.P. Mterenge
Mlandizi Ward, Kibaha District
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of February 20 23 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 20 23

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

Served Upon Me/us:
Name.........................................
Signature.........................................
Qualification/Relationship
Date.........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
(AT KIBAHA)

CRIMINAL CASE NO. 7 OF 20 23

THE REPUBLIC
VERSUS

JUBED WILFRED MAKERE.............................................ACCUSED PERSON

To:
Jubed Wilfred Makere
Matumbi, Kerege, Bagamoyo District
Pwani Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 23 day of February 20 23 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 20 23

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name.........................................
Signature.........................................
Qualification/Relationship
Date.........................................

# Mama, mwanawe wauawa, watenganishwa viungo

**Na Francis Godwin**, IRINGA

WATU wasiojulikana wamemuua mwanamke mkazi wa Kijiji cha Ilambilole, Wilaya ya Iringa mkoani hapo, Anitha Mbilinyi (48) na mwanawe Andrea Mbwilo (7) kwa kutenganisha kichwa, mikono na miguu.

Wakizungumza na Nipashe, mashuhuda wa tukio hilo walisema lilitokea Februari 10, mwaka huu, katika mpaka wa Kijiji cha Ilambilole na Matembo wakati mwanamke huyo na mtoto wake wakitoka shambani kufanya kazi za kibarua.

Rafiki wa marehemu, Elitha Belo, akizungumza na Nipashe, alisema kuwa kabla ya taarifa za vifo hivyo, alikutana na mama huyo na kuzungumza naye na kumwahidi kumlipa deni lake la Sh. 2,000 alilokuwa akimdai.

"Nilikutana na Anitha siku mbili kabla ya kifo chake na aliniomba radhi kwa kuchelewa kunilipa deni la Sh. 2,000 na alisema kuwa Jumapili angelipa, nikamwambia hakuna shaka ila nimesikitishwa kupokea taarifa ya kifo chake cha kinyama," alisema Elitha.

Alisema kuwa baada ya kufika ofisi ya kijiji, walipoelezwa tukio la mauaji ya mwanamke huyo na mwili wake kutelekezwa kando ya barabara ya lami.

Alisema kuwa baada ya kufika eneo hilo, walikuta mwili huo ukiwa hauna kichwa, mguu mmoja na mkono mmoja baada ya watu hao waliotekeleza unyama huo kuondoka na viungo hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya ndugu wa marehemu huyo, mdogo wa marehemu, Jane Mbilinyi alisema kuwa dada yake alikutwa na umauti majira ya saa 12 jioni wakati akirejea kutoka shambani akiwa na mtoto wake aliyekuwa anasoma darasa la pili Shule ya Msingi Ilambilole.

Alidai kuwa wauaji hao walipotekeleza walitokomea na baiskeli ambayo alikuwa ameazima kwa rafiki yake na kwamba hadi leo rafiki yake huyo hajulikani aliko.

"Dada yangu baada ya kuwasiliana kwa njia ya simu alinisisitiza kuwa tuendelee kupambana na maisha ili kulea familia na yeye aliniambia kuwa amepata kazi ya kupalilia mahindi shambani maana maisha ni magumu sana," alisema.

Alidai kuwa mtoto Andrea alimfuata mama yake shambani baada ya kurejea kutoka shuleni majira ya saa tano asubuhi ndipo kifo kilipomkuta huko.

Alisema kuwa ndugu yake huyo alikuwa na watoto watano akiwamo Andrea aliyefariki dunia.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kihesa, Kijiji cha Ilambilole, Angela Nyalusi alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, waliwajulisha wenyeviti wa vitongoji ili kuutambua mwili huo na baadaye miili ilitambulika ikiwa imetenganishwa baadhi ya viungo ikiwamo kitovu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ilambilole, Jeiros Kiuno, alisema tukio hilo ni la kwanza kutokea kijijini huko na kwamba baada ya kutoa taarifa, polisi wanaendelea kuwasaka wahusika.

Alisema mwili wa mama huyo na mwanawe ilichukuliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi na wanatarajia kuizika leo kwenye Kijiji cha Ilambilole.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Allan Bukumbi alipotafuta kwa njia ya simu ili kuzungumzia tukio hilo hakupatikana.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Veronica Kessy, alipotafutwa kwa njia ya simu, alidai alikuwa safarini na kumtaka mwandishi wa habari kuwasiliana na Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa, Stomen Kyando, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba watu wawili walikuwa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa uchunguzi zaidi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, alithibitisha kupokea miili ya marehemu hao.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. ........... OF 20..................

THE REPUBLIC
VERSUS

ABDULQADIR ALLY QUALLATEN.........................................ACCUSED PERSON

To:
Abdulkadir Ally Quallaten
Plot No. 58, Block J, Kurungeni Area
Mafia District, **Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 23rd day of February 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 23rd day of January 2023

..........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

**Served Upon Me/us:**

Name..........................................
Signature.....................................
Qualification/Relationship
Date..........................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 3 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

BOAZ NDAMO.........................................ACCUSED PERSON

To:
Boaz Ndamo
Mapinga Ward, Bagamoyo District
**Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 23 day of February 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 2023

..........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name..........................................
Signature.....................................
Qualification/Relationship
Date..........................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 13 OF 2023

THE REPUBLIC
VERSUS

S.M. HOLDING LIMITED.........................................ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
S.M. Holding Limited
Plot No. 18, Block F,
Mwanambaya Village, Mkuranga
**Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 23rd day of February 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 23rd day of January 2023

..........................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

**Served Upon Me/us:**

Name..........................................
Signature.....................................
Qualification/Relationship
Date..........................................

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF KIBAHA
*(AT KIBAHA)*

CRIMINAL CASE NO. 2 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

SAID ALLI SAID *aka* CHOTARAI.........................................ACCUSED PERSON

To:
Said Alli Said
Ikwiriri Kaskazini, Rufiji District
**Pwani Region**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 23 day of February 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 23 day of January 2023

..........................................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name..........................................
Signature.....................................
Qualification/Relationship
Date..........................................



# Wanufaika wa mikopo ya h'shauri wapata hasara

**Na Godfrey Mushi**, HAI

VIKUNDI vingi vinavyonufaika na mikopo ya asilimia 10 ya uwezeshaji kiuchumi makundi maalum ya wanawake, vijana na jamii ya watu wenye ulemavu, vinadaiwa kuendesha miradi yao kwa hasara kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Hali hiyo inatajwa kama moja ya mambo yanayochangia kusuasa kwa urejeshaji wa mikopo hiyo inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi pikipiki nne za miguu mitatu (guta) na pikipiki tano za abiria (bodaboda) kwa vikundi viwili vya vijana, kikundi kimoja cha wanawake na mtu mmoja mwenye ulemavu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Dionis Myinga, alisema baadhi ya wanufaika hawarejeshi mikopo kutokana na dhana potofu wanazojenga kuwa fedha ni ya serikali na hazipaswi kurejeshwa.

"Hata hivyo, vikundi vingi havina miradi ya pamoja na hivyo kusababisha kugawana fedha za mikopo wanayopewa na kushindwa kufanya marejesho. Lakini kuna baadhi ya vikundi vinaendesha miradi kwa hasara.

"Kwa hiyo, vikundi hivi vinakabidhiwa vitendea kazi kama sehemu ya kuwakilisha vikundi vingine vyote vilivyopokea mikopo hiyo ya Sh. milioni 142.034.

"Katika awamu ya pili, halmashauri itatoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 119.837.

"Kwa sasa kazi ya kuhakiki vikundi vilivyopendekezwa kukopeshwa awamu ya pili imekamilika na kupitishwa na kamati ya mikopo ya halmashauri," alisema.

Baada ya kukabidhi mikopo hiyo, Mbunge wa Hai, Saashisha Mafuwe aliowanya wanufaika wanaotafuta mbinu chafu ya kujificha ili wasirejeshe mikopo hiyo kwa wakati, akisema itafika mahali hataona haya hata kama ni wananchi wake, atamwomba Mkuu wa Wilaya hiyo, Amiri Mkalipa kuwadai kwa nguvu.

Awali Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Robert Mwanga, alisema kuwa kutokana na mikopo iliyotolewa, ajira 142 zimetengenezwa, ambapo kati ya ajira hizo za vikundi, wanawake ni 88, vijana 53 na watu wenye ulemavu watatu.

# RC amkosha waziri upandaji wa miti

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Seleman Jafo, amempongeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, kwa kusimamia kwa dhati operesheni ya upandaji miti kwenye maeneo mbalimbali ambayo yalipoteza uoto wa asili kutokana na ukame.

Amesema mazingira asili yasipotunzwa, mabadiliko ya tabianchi yataleta athari kwa jamii, mifugo na kilimo.

Dk. Jafo alitoa pongezi hizo jana jijini hapo wakati wa uzinduzi wa kitabu cha kwanza cha maarifa ya asili kwenye uhifadhi wa mazingira, misitu na vyanzo maji.

Kitabu hicho kimeandaliwa na Taasisi ya Waandishi wa Habari wa Kusaidia Jamii za Pembezoni (MAIPAC) kwa kushirikiana na Taasisi ya CILAO.

"Lakini mazingira yakitunzwa vizuri kwa kuhakikisha miti inapandwa na kurudisha uoto wa asili, itasaidia kurudisha mvua zisizo na ukomo na kuepukana na mabadiliko ya tabianchi yanayoleta athari kwa jamii.

"Kuhusu mradi huu, ni wa kipekee na ninawapongeza MAIPAC kwa kazi nzuri, kwani pia nimeona makala ya video fupi ikielezea utunzaji wa mazingira na nina imani na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini na wafadhili wengine wataendelea kuwapa fedha zaidi kuendeleza mradi huu lakini vitabu hivi vitagaiwa shuleni na maeneo mengine ili kulinda mazingira," alisema.

Dk. Jafo alisema uhifadhi wa mazingira kwa maarifa ya asili ni muhimu kwa kuwa maarifa hayo yalikuwa yanatumika tangu enzi za 'mababu' na yamesaidia kutunza misitu, vyanzo vya maji na mazingira na kitabu hicho kitakuwa njia sahihi ya kueneza elimu ya utunzaji wa mazingira kwa njia ya asili.

Mkurugenzi Mtendaji wa MAIPAC, Mussa Juma, alisema kitabu hicho kimeelezea simulizi za jamii ya Masai, wanavyotumia taratibu na mila zao katika kutunza mazingira, vyanzo vya maji na misitu.

Alisema mradi huo ulizinduliwa rasmi Agosti 27 mwaka jana jijini Arusha na Mkuu wa Mkoa wa Arusha ambaye aliwakilishwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa Arusha, Blandina Nkini.

Alisema mradi huo umefadhiliwa na Programu ya Miradi Midogo ya Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF) unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) nchini, chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

Katika hafla hiyo, Mratibu wa Miradi Midogo ya UNDP kupitia Shirika la Mfumo wa Mazingira Duniani (GEF), Faustine Ninga, alipongeza shirika hilo kwa kukamilisha kuchapa vitabu na kuandaa video na machapisho ya mradi huo.

# Watumishi 300 kunufaika mafunzo matumizi mtandao

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI za Tanzania na Marekani zimeanza kuwapiga msasa watumishi wapya wa umma zaidi ya 300 kwa kutumia mfumo wa mtandao ili kupunguza gharama ya uendeshaji wa mafunzo na kusaidia shughuli za umma kutokukwama.

Mradi huo wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma Awamu ya Pili (PS3+) unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendelo ya Kimataifa (USAID), una lengo la kuhakikisha watumishi wa umma wanajifunza mbinu mbalimbali za ufanisi kazini.

Akizungumzia mradi huo jana jijini Arusha, Mkurugenzi wa Tathmini Ufuatiliaji na Mafunzo wa mradi wa uimarishaji wa mifumo ya sekta za umma awamu ya pili, Kusekwa Sono alisema mafunzo kwa watumishi wa umma kupitia mradi wa uimarishaji wa mifumo ya sekta yanalenga uimarishaji wa utoaji huduma katika sekta mbalimbali kwa wananchi ili kuhakikikisha maisha ya watu wa chini yanaboreshwa.

Alisema mfumo wa ujifunzaji kielektroniki (MUKI) unaosimamiwa na Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo), unawezesha mshiriki yeyote wa mafunzo kuyapata bila kwenda darasani na kuongeza kuwa mafunzo hayo yanafundishwa kielektroniki bila mhusika kuingia darasani.

Katika kuhakikisha watumishi wengi wa umma wapya wa serikali wanapata mafunzo ya maadili yanayofuata kanuni na sheria za kazi zao, mfumo huo unatajwa kuwa mwarobaini wa gharama za uendeshaji kwa serikali.

Boniphace Luhende ni Ofisa Utumishi Mwandamizi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) alisema mfumo huo utawasaidia watumishi kujua uhusiano kati ya waajiri na watu mbalimbali.


Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Andrea Gunda ambaye ni Ofisa Utumishi wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, alisema mfumo huo umewasaidia kufahamu mipaka ya utendaji mahali pa kazi.

Mafunzo hayo yaliwahusha maofisa utumishi kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.


RTI INTERNATIONAL

## Request for Quotation/Proposal (RFQ/RFP)

| | |
|---|---|
| **Commodity/Service Required:** | Provision of Vehicle Hire Services (Passengers vehicle) |
| **Scope of Work:** | RTI International's Act to End Neglected Tropical Diseases (NTDs) \| East program in Tanzania is funded through USAID. Act to End NTDs \| East supports Tanzania's MoH to reach their NTD control and elimination goals through proven, cost-effective public health interventions.<br><br>Act to End NTDs \| East Tanzania project implemented by RTI international is seeking offers from reputable, well established, and experienced Car Hire Firms duly incorporated in Tanzania to provide vehicle transportation Services for RTI Act to End NTDs \|East Tanzania staff members or assigned non-staff; at a fixed price for a period of one year renewable for an additional year based on satisfactory performance. |
| **Type of Procurement:** | Provision of vehicle hire services for period ending Aug 31 2023 with a possibility of awarding Master Service Agreement (MSAs) until April 2024, and with a possibility of renewing for an additional one year subject to satisfactory performance. |
| **Type of Contract:** | Master Service Agreement |
| **Term of Contract:** | Provision of vehicle hire services for period ending Aug 31, 2023, with a possibility of awarding Master Service Agreement (MSAs) until April 2024, and with a possibility of renewing for an additional one year subject to satisfactory performance. |
| **Contract Funding:** | USAID |
| **This Procurement supports:** | RTI – Act to End NTD's \| East Tanzania Project |
| **Request RFP document from:** | lanyisile@rti.org and tmwakasege@rti.org<br>CC wmhando@rti.org |







Mkurugenzi wa Sera na Mpango TAMISEMI, John Cheyo (mwenye kofia), akitembelea moja ya wodi ya kituo cha afya cha Bugarama wakati ujumbe wake ulipotembelea miradi mbalimbali iliyotekelezwa kwa fedha za uwajibikaji kwa jamii (CSR) zilizotolewa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu mwishoni mwa wiki. Wengine ni wafanyakazi wa Barrick Bulyanhulu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yajivunia mafanikio ya Sekondari ya Nyankumbu

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAKATI wakuu wa mikoa na wilaya wakihaha kuhamasisha wazazi wawapeleke watoto wao shuleni kujiunga na kidato cha kwanza, Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu imezidiwa kwa wingi wa maombi ya wazazi kuwapeleka watoto wao kwenye shule hiyo kutokana na ufaulu mzuri na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Shule hiyo ya serikali iliyojengwa na kuzinduliwa mwaka 2014 na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita kupitia fedha za Mfuko wa Uwajibika wa Kampuni kwa Jamii (CSR), imetajwa kuwa mkombozi kwa wanafunzi wa kike kwenye mkoa huo.

GGML ilitumia Sh. bilioni 15 katika ujenzi wa shule hiyo ya bweni pamoja na kuboresha miundombinu ya shule nyingine za mkoa huo kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha Sekta ya Elimu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Shule hiyo, Georgia Mugashe alibainisha kuwa mwaka huu wa masomo, wamesajili wanafunzi wapya wa kidato cha kwanza 240 huku wakishindwa kuchukua wengine kutokana na wingi wa maombi.

Alisema shule hiyo yenye wanafunzi zaidi ya 1,050, imekuwa mkombozi kwa jamii ya wanaGeita kutokana na mwenendo mzuri wa matokeo ya shule katika mitihani ya kidato cha nne na mazingira mazuri ya kusomea ikiwamo miundombinu bora iliyojengwa na GGML.

Alirejea matokeo ya kidato cha nne ya mwaka jana ambayo wanafunzi wote wamefaulu na hakuna aliyepata daraja sifuri.

"Jumla ya wanafunzi 38 walipata daraja la kwanza, 86 daraja la pili, 36 daraja la tatu na sita daraja la nne. Kwa hiyo, unaona namna tunavyopambana kuhakikisha wote wanapata daraja la kwanza kwa sababu hata katika matokeo ya mwaka juzi, yaani 2021, waliopata daraja la kwanza walikuwa 50.

"Tunawashukuru sana GGML kwa sababu huwezi kuamini hii ni shule ya serikali kutokana na huu mwamko wa wazazi kuleta watoto wao hapa.

"Na hakuna kingine zaidi kinachowavutia, ni ufaulu mzuri na mazingira mazuri ya kusoma, kwani wazazi hupenda watoto wakae bweni," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na mwamko huo, idadi ya wanafunzi imeongezeka hadi shule kuzidiwa kwani mabweni yaliyopo sasa hayatoshi.

Aliwaomba wadau wengine kujitokeza kuendelea kuunga mkono serikali na GGML katika kuboresha mazingira ya shule hiyo.

Akizungumzia matokeo hayo, Makamu Rais wa Anglo-Gold Ashanti anayesimamia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo alisema inafurahisha na kutia moyo kuona shule ambayo GGML imeianzisha kwa lengo la kuboresha elimu mkoani Geita, inafanya vizuri na kuwa kivutio kwa wazazi.

Alisema GGML imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za serikali, ikijenga miundombinu kwenye shule za Bugando na Kamena ambazo zimeanza kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita kuanzia mwaka 2021/22.

"Kwenye shule hizi mbili tulitumia Sh. milioni 287.5 na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Geita, fedha hizi zilitolewa kupitia CSR," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule kwa upande wa wazazi, Eliangikaya Mshana, pia aliishukuru GGML kwa kuendelea kuungana na wazazi pamoja na jamii ya Geita kuboresha mazingira ya elimu mkoani hapo hadi kuwezesha shule hiyo kuwa moja ya shule ya mfano mkoani Geita.

# Madiwani waitaka serikali kutoa mahindi ya bei nafuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga wameitaka serikali kuendelea kutoa na kuuza mahindi ya bei nafuu kwa wananchi ili kuwanusuru na upungufu wa chakula uliopo.

Wamesema hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu hasa kwa wananchi wa hali ya chini ambao hawana vyakula, baadhi wanalazimika kupata mlo mmoja kwa siku.

Kilio hicho cha wawakilishiwa wananchi kilisikika kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wiki iliyopita, wakisisitiza kuwa hali inazidi kuwa mbaya.

Kutokana na hali hiyo, waliitaka serikali kuendelea kutoa mahindi ya msaada ya bei nafuu ili kuwanusuru wananchi kukumbwa na njaa.

"Tunaitaka serikali iendelee kuleta chakula cha bei nafuu na kuwauzia wananchi maana hali ni mbaya," alisema Diwani wa Kitangili, Mariam Nyangaka.

Madiwani hao pia walikiri serikali imetoa fedha nyingi ili kutekelezwa miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Hata hivyo, walisema kuna kero ambazo bado zinahitaji kutatuliwa ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, upungufu wa matundu ya vyoo na walimu shuleni na kuchelewa ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alisema kero zote ambazo zimewasilishwa kwenye baraza hilo la madiwani zitafanyiwa kazi na baadhi tayari zipo kwenye utekelezaji.

# Wananchi wafundwa kutoa taarifa ukatili kijinsia

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MHADHIRI wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Jumanne Homera, ameitaka jamii mkoani Kagera kutoa taarifa kwenye vyombo vya sheria pale inapoona vitendo vya ukatili wa kijinsia ili kuvikomesha.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipowasilisha taarifa ya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kwenye kikao cha tathmini ya shughuli ya mpango wa utekelezaji wa robo mwaka kwenye wilaya za Mkoa Kagera.

Kikao hicho kilijumuisha wadau kutoka taasisi mbalimbali ndani, Dk. Homera akisema kunapaswa kuwapo ushirikiano wa jamii yenyewe, taasisi za elimu, afya na dawati la jinsia la Jeshi la Polisi ili kukabiliana tatizo hilo.

Alisema wazazi ndiyo wenye majukumu makubwa ya kuangalia mienendo ya hatua za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto kwenye jamii ambako matukio ya kikatili huanzia.

Alisema kazi ya taasisi ni kutoka tathmini ya matokeo ya kazi zinazofanywa na ujumuishi wa mpango wenyewe na pia wataalamu ambao wataboresha elimu kutokana na mitaala itakayotolewa.

"Sisi tutatoa wataalamu ambao watakuja kufundisha jamii mpango huo wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto unaoangalia jamii yenyewe," alisema Dk. Homera.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Leah Mwakajombe, alisema mpango huo umejumuisha makundi maalum wakiwamo watu wenye ulemavu na watoto waliopo kwenye mazingira hatarishi kwa kuunganisha na afua mbalimbali.

Alisema tathmini za mkoa zinaonyesha kuna sababu mbalimbali zinazotokea katika makundi hadi watoto kuingia na kuishi kwenye mazingira magumu.

"Wazazi kutokuwa na uwezo wa kiuchumi na kushindwa kulea watoto wao ni sehemu ya tatizo, sasa kama wizara tunakuja na mpango wa kusaidia wanawake kiuchumi ili waweze kujishughulisha na kupata njia za kulea watoto wao," alisema Mwakajombe.

Ofisa wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia, Suzan Kaganda, alisema wamekuwa wakitembelea jamii na kutoa elimu ya ukatili kwa watoto ikiwamo kuangalia ulinzi na usalama wao.


Alisema tayari dawati lake limepokea kesi 13 kuanzia mwezi Januari mwaka huu hadi sasa ambazo zinahusisha vitendo vya ukatili wa aina mbalimbali.

Alisema hulazimika kufanya doria na kutembelea sehemu za mikusanyiko ili kuangalia wazazi waliopo maeneo hayo na kutoa elimu.

Nipashe Spotika




NINI CHA KUTARAJIA KUTOKA MADRID 2022/23 UK. 12-13




JORGINHO

# WAKALI WATANO WALIOSAJILIWA JANUARI

**LONDON,** England

DIRISHA la usajili la msimu wa baridi wa 2022/23, lilikuwa la kukumbukwa kwani klabu za Ligi Kuu England, haswa Chelsea, zilitumia fedha nyingi kwa wachezaji wapya. Hata hivyo, si wao pekee walionyakua vichwa vya habari huku klabu kutoka sehemu mbalimbali za dunia zikipiga hatua zisizotarajiwa kwenye soko la uhamisho.

Usajili wa Januari mara nyingi hujumuisha wachezaji waliosajiliwa ili kuziba pengo kwenye kikosi. Lakini dirisha la usajili la 2022/23 lilishuhudia klabu nyingi zikiwasajili nyota wa kikosi cha kwanza ama kwa mkopo au kwa mikataba ya kudumu, ambayo ilishangaza sana.

Kwa kuzingatia hilo, wacha tuangalie usajili wa wachezaji wakali watano waliosajiliwa wakati wa dirisha la usajili la Januari 2023, tende sasa...

**#5. Marcel Sabitzer kwenda Manchester United**

Manchester United ilitoa Euro milioni 243 katika dirisha la usajili la majira ya joto msimu huu ili kuimarisha kikosi cha kocha mpya Erik Ten Hag.

Pia walimwongeza Wout Weghorst kikosini mapema mwezi uliopita ili kutoa makali ya ziada ya mashambulizi kwenye eneo la hatari.

Jack Butland pia alisajiliwa kwa mkopo kutoka Crystal Palace ili kumsaidia David de Gea. Kila mtu aliamini kuwa huo ulikuwa mwisho wa biashara ya msimu wa baridi ya uhamisho wa klabu, lakini jeraha la Christian Eriksen liliwalazimisha kuingia sokoni.

Kiungo huyo wa Denmark huenda akakaa nje kwa miezi mitatu, hivyo basi kuacha pengo kubwa kwenye safu ya kiungo kwa 'Mashetani Wekundu' hao, hivyo waliishia kumsajili Marcel Sabitzer kutoka Bayern Munich kwa mkopo siku ya mwisho ya dirisha la usajili.

Kiungo huyo aliyejiunga na Bavaria mwaka 2021, hakuweza kuwa kwenye nafasi katika kipindi cha miezi 18 iliyopita. Kuna ushindani mkubwa katikati ya uwanja, Joshua Kimmich, Ryan Gravenberch, Jamal Musiala na Leon Goretzka mara nyingi hukuchaguliwa kuanza. Hivyo uhamisho huu ulikuwa wa maana kwa Bayern, kwani hakuna chaguo la kununua lililojumuishwa katika mpango huo.

Bila kujali, Manchester United imesajili mchezaji ambaye anaweza kufanya vema kwenye ncha zote mbili za uwanja, jambo muhimu katika kuchezea kikosi cha Ten Hag siku hizi.

**#4. Jorginho kwenda Arsenal**

Jorginho ulikuwa uhamisho mwingine wa siku ya mwisho kwani raia huyo wa Italia mzaliwa wa Brazil alihama kutoka London Magharibi hadi London Kaskazini kujiunga na Arsenal kwa pauni milioni 11.

Mshindi huyo wa Euro 2020 alikuwa amebakiza chini ya miezi sita katika mkataba wake pale Stamford Bridge, bila dalili za klabu hiyo kumpa nyongeza ya muda. Kwa kuzingatia matumizi makubwa ya Chelsea katika uhamisho wa wachezaji msimu huu, uuzaji wa mchezaji aliyezeeka ulikuwa wa maana kwao. Hata hivyo, hii inaweza kuwa faida kwa Arsenal kwani walijizatiti kumsajili mchezaji huyo baada ya kushindwa kumnasa Moises Caicedo.

Jorginho anaweza kuamuru kucheza, kumiliki mpira na kutengeneza nafasi. Yeye pia ni sauti kubwa katika chumba cha kubadilishia nguo na anaweza kuwa kiongozi pale Arsenal.

**#3. Mykhaylo Mudryk kwenda Chelsea**

Chelsea inaweza kuwa imemuuza mmoja wa viongozi wao, Jorginho kwa Arsenal siku ya mwisho, lakini hii ilikuwa tu baada ya kumpata Mykhaylo Mudryk.

'Washikabundi' hao walikuwa wakiwinda saini ya raia huyo wa Ukraine tangu majira ya joto yaliyopita na walizidisha juhudi zao Januari kutaka kumsajili. Hata hivyo, ofa zao zote tatu zilikataliwa na Shakhtar Donetsk.

Chelsea, ambao pia walikuwa wakimtaka mchezaji huyo, walisonga haraka, huku mmiliki mwenza Behdad Egbahli na mkurugenzi mwenza wa michezo, Paul Winstanley, wakisafiri kwa ndege kuelekea Uturuki kukamilisha mpango huo.

**#2. Cristiano Ronaldo kwenda Al Nassr**

Ikiwa mtu angemwambia Cristiano Ronaldo miezi sita iliyopita kwamba angeichezea Al Nassr mwaka 2023, fowadi huyo wa Ureno angecheka.

Hata hivyo, nyota huyo aliyetwaa tuzo ya Ballon d'Or mara tano sasa anaongoza kwenye mstari wa klabu hiyo ya Saudi Arabia baada ya kukatisha mkataba wake na Manchester United Novemba mwaka jana. Mvutano kati yake na Mashetani Wekundu ulikuwa wazi tangu majira ya joto na ripoti kadhaa zikionyesha kuwa mshambuliaji huyo alikuwa akitafuta kuondoka.

Kutofautiana kwake na Erik ten Hag pia kulikua zaidi ya miezi iliyofuata, ambayo baadaye alielezea kwa undani wakati wa mahojiano na Piers Morgan. Mahojiano hayo ambayo yalitolewa wiki moja kabla ya Kombe la Dunia la FIFA 2022, yalipelekea Man United kuamua kuachana na mchezaji huyo.

Lakini kutokana na matokeo mabaya ya Kombe la Dunia, Ronaldo aliishia kusaini karatasi za Al Nassr. Mkataba wake unaripotiwa kuwa na thamani ya zaidi ya euro milioni 200.

**#1. Joao Cancelo kwenda Bayern Munich**

Ni usajili ambao haukutarajiwa na ni vigumu kuelewa jinsi Manchester City walivyohalalisha kuruhusu Joao Cancelo kuondoka kwa mkopo.

Beki huyo wa kulia wa Ureno, ambaye bila shaka amekuwa beki bora zaidi wa kulia katika soka la dunia mwaka uliopita, alijiunga na Bayern Munich siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho la Januari.

City mara nyingi huweka vikwazo kwa wachezaji wasiopenda kuwachezea, lakini hilo hutokea mara chache katika dirisha la usajili la majira ya baridi. Zaidi ya hayo, klabu hiyo bado iko kwenye kinyang'anyiro cha kuwania taji la Ligi Kuu England, bila kusahau pia kuwa na matumaini ya kukamilisha harakati zao za kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Baada ya kukamilisha uhamisho wa siku ya mwisho wa kuhamia Bayern Munich, Joao Cancelo amejibu tetesi kuwa alikosana na Pep Guardiola katika klabu ya Manchester City.

Wakati Nathan Ake, Kyle Walker na Rico Lewis wamecheza nafasi ya beki kwa ustadi, tishio la Cancelo kwenda mbele halina kifani. Kwa hivyo, ilichanganya zaidi kwa nini beki wa kulia aliwekwa benchi kwa mechi nyingi kama alivyokuwa mwezi uliopita.

Bila kujali, Bayern Munich, ambao wamemsajili kwa mkopo na chaguo la kumnunua kwa Euro milioni 70, watafurahishwa na uhamisho huu. Beki huyo alitoa pasi ya mabao katika mechi yake ya kwanza katika klabu hiyo hivi majuzi na hivyo kuashiria kwamba anaweza kupiga hatua kuwania mabingwa hao watetezi wa Bundesliga.

## ISIKUPITE

KATIKA ligi tano bora Ulaya Premier League, LaLiga, Serie A, Bundeslinda na Ligue 1, Lionel Messi (697), ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi akifuatiwa na Cristiano Ronaldo (696), Robert Lewandowski (470), Karim Benzema (402) na Zlatan Ibrahimovic (391). Idadi hiyo ya mabao ni pamoja na yale waliyofunga kwenye michuano ya makombe mbalimbali ya mashindano ya ndani na barani humo.



## Extra Time



# NINI CHA KUTARAJIA KUTOKA KWA REAL MADRID 2022/23

**MARID,** Hispania

REAL Madrid, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Hispania na Ulaya, huwa wanatarajiwa kushinda kila mashindano wanayoshiriki. Msimu huu si tofauti kwani Kocha Carlo Ancelotti atakuwa akitafuta kunyakua angalau mataji mawili makubwa baada ya kubeba taji la Klabu Bingwa Dunia juzi kwa kuifunga Al Hilal ya Saudi Arabia kwa mabao 5-3 katika mchezo wa fainali uliopigwa Morocco.

**Ligi ya Mabingwa Ulaya ni shindano ambalo 'Los Blancos' wana rekodi ya kushangaza na mabingwa hao watetezi wanatarajia kurudia ushujaa wao wa msimu uliopita. Ancelotti pia atajaribu kumaliza ukame wa klabu hiyo wa Copa Del Rey.**

Mashabiki wa Madrid wangependa kuona timu yao ikinyanyua Kombe la Copa del Rey mwaka huu.

Mwaka huu unaweza kuwa hadithi tofauti kwani tayari wako kwenye fainali ya shindano hilo dhidi ya Barcelona Machi 2, mwaka huu.

Los Blancos hao walifedheheshwa na Barcelona walipopoteza kwa mabao 3-0 kwenye Supercopa de Espana mapema mwezi huu.

### LIGI YA MABINGWA ULAYA

Real Madrid walikuwa na moja ya mbio bora zaidi katika Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita huku wakizishinda timu zote bora kwenye dimba hilo na kushinda taji hilo kwa mara ya 14.

Uchezaji wao msimu huu umekuwa wa kuridhisha pia, kwani waliongoza kundi lao. Madrid itacheza na Liverpool katika Raundi ya 16-Bora katika mechi ya marudiano ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2022, ambayo Los Blancos ilishinda 1-0. Mechi ya kwanza itachezwa Februari 21 kwenye Uwanja wa Anfield.

### LALIGA

Ligi Kuu Hispania, LaLiga imeonekana kushuka kwa ubora katika miaka michache iliyopita tangu Cristiano Ronaldo na Lionel Messi waondoke. Barcelona na Real Madrid ziko katika kinyang'anyiro cha kuwania taji la ligi msimu huu.

Real Madrid ilishinda LaLiga kwa raha msimu uliopita ikiwa na faida ya pointi 13 dhidi ya Barcelona. Mwaka huu, wanaburuza mkia kwa Barca kwa pointi nane kabla ya mechi za jana.

Ingawa Madrid waliwashinda Barcelona kwa raha katika mechi yao ya LaLiga, wamepoteza pointi mara nyingi sana. Barca hawaonyeshi dalili za kupunguza kasi, hivyo Real Madrid wanatakiwa kuwa katika ubora wao ili kuendelea kuwa karibu na wapinzani wao hao.

### WACHEZAJI WANAOWAHITAJI

Vinicius Junior na mshindi wa Ballon d'Or, Karim Benzema ndio silaha kubwa zaidi kwa Real Madrid. Watalazimika kuendelea kucheza kwa kiwango sawa na msimu uliopita ikiwa wanataka timu yao kufikia mafanikio.

Vinicius alionyesha dalili za wasiwasi katika sehemu za mwanzo za msimu, lakini winga huyo amerejea kufanya kile anachofanya vema zaidi. Benzema amekuwa butu tangu kuumia kabla ya Kombe la Dunia. Amefunga mabao tisa kwenye LaLiga, manne chini ya mabao 13 ya Lewandowski. Itakuwa vigumu kwake kushinda tuzo ya mfungaji bora (Pichichi) kwa kasi hii.

Hata hivyo, anazidi kushika kasi na bao lake dhidi ya Atletico Madrid katika robo fainali ya Copa del Rey hakika litampa nguvu ya kujiamini. Thibaut Courtois yuko katika kiwango kizuri, kama vile msimu uliopita, ambao ulikuwa bora kwake binafsi.

### KIWANGO

Los Blancos wameshuka ghafla katika hali yao tangu mapumziko ya Kombe la Dunia. Walichapwa na Villarreal na FC Barcelona katika muda wa siku tisa. Real Madrid walipata ushindi usioridhisha dhidi ya Real Valladolid, CP Cacereño na Valencia.

Walishinda 2-0 dhidi ya Athletic Bilbao wakiwa ugenini, ambayo ni mafanikio makubwa ukizingatia kiwango chao cha hivi majuzi na walitoka suluhu na kufanya matokeo kuwa 3-1 dhidi ya Atletico Madrid.

Kuna baadhi ya masuala ambayo Ancelotti anahitaji kutatua haraka iwezekanavyo. Vinicius anatengwa mara nyingi sana kwenye ubavu wa kushoto na Ferland Mendy anapaswa kufanya zaidi kumsaidia katika kushambulia. Pia Rodrygo anastahili kupata muda zaidi wa mchezo.

## Nukuu

"Nataka timu ijue ni jinsi gani ninawapenda. Nawapenda sana kuliko saa tatu zilizopita, wiki moja iliyopita, mwezi uliopita, miezi mitatu iliyopita. Ni rahisi sana kuwa karibu na wachezaji wanaposhinda na kufanya vizuri. Huu ndio wakati ninawapenda wachezaji wangu zaidi, wafanyakazi zaidi na sasa tunashikamana pamoja," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta baada ya kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Everton wiki moja iliyopita.**



"Hakuna mtu anayeweza kuiondoa, hisia, wakati mzuri, wakati mbaya. Mafanikio ya Manchester City siku zote yatakuwa yetu hata kama klabu itanyang'anywa mataji yake ya Ligi ya Kuu England," **Kocha Man City, Pep Guardiola, wakati huu klabu hiyo ikishtaki kwa ukiukaji zaidi ya 100 wa sheria zake za kifedha kati ya mwaka 2009 na 2018.**



"Hakika uwapo wa Ronaldo [Cristiano] unafanya mechi kuwa ngumu zaidi kwetu kwani timu zote zinatafuta kushiriki dhidi yake kwa njia bora zaidi, na anatoa motisha kwa kila mtu," **Kiungo wa Al-Nassr, Luiz Gustavo, akieleza jinsi ujio wa Ronaldo ulivyofanya maisha kuwa magumu kwa vinara hao wa ligi kuu ya Saudia. Kikosi hicho cha Kocha Rudi Garcia kimeshinda mechi mbili tu kati ya nne ambazo mshambuliaji huyo amecheza.**






Straika wa Yanga, Fiston Mayele, kinara wa mabao Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 22. **NA MPIGAPICHA WETU**

# REKODI, TAKWIMU LIGI KUU RAUNDI YA 22 KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

ZIMEBAKIA raundi nane tu kabla ya kutamatika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 ambayo ipo kwenye raundi ya 22 sasa, jana kulikuwa na mechi moja tu ya raundi ya 23 kati ya Ihefu dhidi ya Singida United, huku mechezo mingine ikitarajiwa kuendelea Ijumaa ijayo.

**Wakati ligi ikiwa raundi ya 22, kuna rekodi nyingi na takwimu zimewekwa na wachezaji pamoja na timu 16 zinazoshiriki.**

Katika makala haya tumekusanya takwimu na rekodi mbalimbali za ligi ambazo zimewekwa mpaka kufikia raundi ya 22 na kuziandika kwa mtindo wa namba...

**59.** Ni pointi inazomiliki Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ikiwa bado iko kileleni mwa msimamo.

**54.** Simba imepachika idadi hii ya mabao kwenye Ligi Kuu, ikiwa ndiyo timu iliyofunga mabao mengi zaidi mpaka sasa.

**53.** Hizi ni pointi za Simba ilizonazo mpaka sasa kwenye ligi na inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo huo.

**43.** Azam FC wana idadi hii ya pointi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, lakini Singida Big Stars ina idadi hii ya pointi, lakini zinaweza kubadilika baada ya mechi ya jana kati ya timu hiyo dhidi ya Ihefu.

**41.** Yanga wamefunga idadi hii ya mabao kwenye Ligi Kuu ambapo inakamata nafasi ya pili kwa kupachika mabao mengi baada ya Simba.

**36.** Hii ni idadi ya mabao walioyonayo Azam FC kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ikiwa ni timu inayoshika nafasi ya tatu kwa kuwa na mabao mengi.

**32.** Hii ni idadi ya mabao ambayo timu za Polisi Tanzania na Mtibwa Sugar zimeruhusu kwenye nyavu zao, zikiwa ndiyo timu zilizoruhusu mabao mengi mpaka sasa. Polisi Tanzania kama ikiruhusu bao lolote leo iwe matokeo ya sare, kushinda au kufungwa dhidi ya Kagera Sugar, itaongoza kwa kupachikwa mabao mengi.

**31.** Ni pointi za Geita Gold ilizonazo mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa kwenye nafasi ya tano ya msimamo.

**30.** Prisons inashika nafasi ya pili kwa kufungwa mabao mengi, ikiwa imeruhusu idadi hii ya mabao kwenye ligi mpaka sasa.

**29.** Baada ya kuibugiza Dodoma Jiji mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Mtibwa Sugar imevuna idadi hii ya pointi kwenye Ligi Kuu, ikiikuta Namungo FC ambayo ilibakiwa na idadi hii ya pointi baada ya kubugizwa mabao 2-0 dhidi ya Yanga, mechi iliyochezwa Februari 4.

**28.** Ni idadi ya mabao ambayo imeruhusu timu ya Coastal Union kwenye nyavu zao mpaka sasa.

**27.** Ni idadi ya mabao ambayo Dodoma Jiji wameruhusu mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa kwenye nafasi ya 11 na pointi zake 24.

**26.** Hii ni idadi ya pointi ilizonazo Kagera Sugar, ambayo inashika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo.

**25.** KMC na Ruvu Shooting wameruhusu idadi hii ya mabao kila moja kwenye Ligi Kuu mpaka kufikia raundi ya 22.

**24.** Hizi ni pointi za Dodoma Jiji na Mbeya City kwenye ligi, lakini Mbeya City ikiwa juu ya msimamo wa mwenzake kwenye nafasi ya 10 na Dodoma Jiji 11 kwa tofauti ya wingi wa mabao.

**23.** Ni pointi za KMC ilizonazo mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa kwenye nafasi ya 12 ya msimamo.

**22.** Hii ni idadi ya raundi ambazo Ligi Kuu imefikia mpaka sasa, pia Prisons ina idadi kama hii ya pointi ikiwa kwenye nafasi ya 13.

**21.** Yalikuwa ni mabao ya kufunga ya Ihefu kabla ya mechi ya jana jioni dhidi ya Singida Big Stars, kama hawakupata bao lolote basi yanabaki yalivyo.

**20.** Haya ni mabao ya kufunga ya timu za KMC na Kagera Sugar zimefunga idadi hii kila moja.

**19.** Yanga wameshinda mara 19, ikiwa juu kileleni mwa msimamo mpaka sasa.

**18.** Ni mabao ya kufunga kwa timu za Prisons na Coastal Union zikiwa pia zinafuatana kwenye msimamo, Wajelajela wakishika nafasi ya 13 na Wanamangusi ya 14.

**16.** Hii ni dadi ya mechi ilizoshinda mpaka sasa ikiwa kwenye nafasi ya pili ya msimamo.

**15**. Fiston Mayele, straika wa Yanga amefunga idadi hii ya mabao na ndiye anayeongoza mpaka sasa kwenye ligi.

**14.** Ni idadi ya pasi za mwisho za kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama ambaye anaongoza kwa 'assist' mpaka sasa.

**13.** Namba hii inasimama kama idadi ya mechi ambazo kipa wa Yanga, Djigui Diarra amekaa langoni bila kuruhusu wavu wake kutikisika 'clean sheets'.

**10.** Haya ni mabao ambayo Yanga imeruhusu kwenye wavu wake, ikiwa ndiyo timu iliyosuruhu mabao machache zaidi mpaka sasa kwenye ligi.

**9.** Ni idadi ya mechi ilizopoteza Namungo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ikiwa na pointi 29 kwa sasa.

**8.** Namba hii inasimama kwa timu ndugu, Kagera Sugar na Mtibwa Sugar. Kila moja imepoteza idadi hii.

**7.** Dodoma Jiji, Mtibwa Sugar, Geita Gold, Mtibwa Sugar ni idadi ya mechi zilizoshinda.

**6.** Ni idadi ya penalti ambazo Dodoma Jiji imepata kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, ikiwa ndiyo timu iliyozawadiwa matuta mengi zaidi mpaka sasa.

**5.** Mohamed Hussein 'Tshabalala' wa Simba ndiye beki anayeongoza kwa 'assist' kwenye Ligi Kuu, akiwa ametoa pasi za mwisho mara tano.


**4.** Ni idadi ya mechi za kushinda kwa timu za Ruvu Shooting na Coastal Union hadi kufikia raundi ya 22.

**3.** Polisi Tanzania ambayo inaburuza mkia, ndiyo timu pekee iliyoshinda mechi chache kwenye Ligi Kuu, ikishinda mara idadi hii.

**2.** Yanga na Ihefu zimetoka sare mara idadi hii kwenye ligi, zikiwa ni chache zaidi, lakini kwa Ihefu itaendelea na rekodi hii kama itafungwa au kushinda kwenye mechi yake dhidi ya Singida Big Stars iliyotarajiwa kuchezwa jana.

**1.** Yanga na watani zao, Simba, zimepoteza mechi chache zaidi kwenye ligi, kila moja ikipoteza mara moja.

## JE, WAJUA?



HARRY Kane ndiye mfungaji bora wa Tottenham wa wakati wote akiwa ameifungia mabao 267, lakini ni mmoja kati ya wachezaji watatu, Alan Shearer na Wayne Rooney ambao wamefunga mabao 200 na zaidi kwenye Ligi Kuu England. Pia Kane ameungana na Rooney kuwa wachezaji wawili walioifungia England mabao mengi zaidi, kila mmoja akicheka na nyavu mara 53.



# Ujenzi wa vivuko vipya waiva

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Umeme na Ufundi Tanzania (TEMESA) umetia saini mikataba mitano ya ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya-Rugezi, Ijinga-Kahangala, Bwiro-Bukondo, Nyakarilo-Kome na Mafia-Nyamisati yenye thamani ya Sh. bilioni 33.2.

Vilevile, wakala huo umebainisha kuwa hadi kufikia mwezi Januari mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 10.3 zimeshalipwa kama malipo ya awali na ujenzi wa vivuko hivyo unaendelea.

Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Lazaro Kilahala, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipotoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli zao kwa waandishi wa habari.

Alisema wakala huo kwa sasa unakamilisha taratibu za ununuzi wa Kivuko cha Buyagu-Mbarika na 'Sea Taxi' mbili. "Wakala umetia saini mikataba 16 ya ukarabati wa vivuko yenye thamani ya Sh. bilioni 23.3 ambapo hadi kufikia mwezi Januari 2023, jumla ya Sh. bilioni 7.96 zilikwishalipwa na kazi zinaendelea," alisema.

Alibainisha kuwa ukarabati wa vivuko sita kati ya hivyo - MV. Kazi, MV. Musoma, MV. Kilambo, MV. Sabasaba, MV. TEMESA na MV. Tanga umekamilika.

Pia alisema wakala umetia saini mikataba 11 ya ujenzi na ukarabati wa maegesho na miundombinu ya vivuko yenye thamani ya Sh. bilioni 4.12 ambapo hadi kufikia mwezi Januari mwaka huu, jumla ya Sh. bilioni 1.79 zilikwishalipwa na kazi zinaendelea.

Pia alisema wakala umesaini mikataba mitano ya ukarabati wa karakana na mikataba miwili ya ujenzi wa karakana mpya za mikoa ya Simiyu na Dodoma yenye thamani ya Sh. bilioni 7.44 ambapo hadi kufikia mwezi Januari mwaka huu, jumla ya Sh. milioni 830.5 zilikwishalipwa.

"Ujenzi wa Karakana ya Simiyu umekamilika na wakala unaendelea na taratibu za ununuzi ili kuanza ujenzi wa karakana za Geita na Njombe," alifafanua.

Alisema wakala pia umetia saini mikataba miwili ya ununuzi na usimikaji wa mifumo ya kielektroniki yenye thamani ya Sh. milioni 910.8 ambapo hadi kufikia mwezi Januari mwaka huu, jumla ya Sh. milioni 435.8 zimekwishalipwa.

"Usimikaji wa mfumo wa Ncard kwenye Kituo cha Magogoni-Kigamboni umekamilika," kiongozi huyo wa wakala alisema.

Alisema kuwa kwa ujumla, hadi kufikia mwezi Januari mwaka huu, wakala umetia saini mikataba ya utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 71.96 ambapo jumla ya Sh. bilioni 23.65 zimekwishalipwa.

"Na kati ya fedha hizo, jumla ya Sh. bilioni 15.625 zimetolewa na serikali ndani ya mwaka huu wa fedha. Kiasi kilichobaki kitaendelea kulipwa kadri utekelezaji unavyofanyika na hati za madai kuwasilishwa," alisema.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabyato (kulia), akizungumza katika semina ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Madini na Nishati, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Adai mke, mtoto kutoweka mazingira yenye utata

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NOEL Mlonga, maarufu Kawawa, mkazi wa Nzuguni A jijini Dodoma, anamtafuta mkewe, Agnes Mapepele (36) (pichani kulia) na mwanawe, Mariam Noel (3) waliotoweka katika mazingira yenye utata takribani mwezi mmoja na nusu sasa.

Akizungumza kwenye ofisi za Nipashe jijini hapo jana, Kawawa alidai mkewe alitoweka Desemba 24, mwaka jana, wakiwa nyumbani kwao Nzuguni A na tangu siku hiyo hapatikani anapopigiwa simu.

"Tumeshafanya juhudi sana na ndugu zangu na ndugu zake kuwatafuta, lakini tumeshindwa kujua walipo kwani simu za mke wangu hazipatikani, hivyo kunipa shaka mahala aliko pamoja na mtoto," alidai Kawawa.

Aliendelea kudai kuwa hiyo ni mara ya pili kwa mke wake kuondoka nyumbani ingawa awali aliondoka bila kuaga lakini alipatikana Chanika mkoani Dar es Salaam na kurejeshwa mikononi mwa polisi akiwa mtoto wake.

"Mke wangu ana akili timamu kabisa, hata kuondoka kwake kwa sasa ninadhani huenda kuna mwanamume kamrubuni, lakini ninaomba wanaofahamu alipo wanitaarifu kutokana na kutoa taarifa Kituo Kikuu cha Polisi Dodoma," alisema. Kawawa alisema kuwa baada ya kuripoti polisi, walimfungulia jalada namba DOM/RB/1986/2023 na kuomba yeyote mwenye taarifa awasiliane kwa simu namba 0753492894 au kituo cha polisi kilichoko karibu.



# DASPA yatoa mbinu kushawishi vijana ili wawe wakulima

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mtendaji wa Shirika la Agriculture Seeds Production Association (DASPA) ameishauri serikali kuwekeza kilimo cha teknolojia kwa vijana kuanzia kuandaa mashamba, kulima, kupanda na kuvuna ili kuwavutia wengi wakipende na kukifanya sehemu ya maisha yao.

Aithan Chaula alitoa rai hiyo jana jijini hapa, akisema matumizi ya teknolojia yanafanya kilimo kiwe rahisi na uzalishaji kuwa mkubwa.

"Kwa mfano shambani kwangu ninalima kilimo cha karanga na mtama kwa kutumia teknolojia mbalimbali katika kuandaa mashamba, kulima, kuvuna, sasa ninategemea kuwa na teknolojia mpya ya mashine ya kuchambua karanga kulingana na madaraja na kutumia teknolojia rahisi," alisema.

Katibu huyo alisema kuwa katika kuandaa mashamba, anatumia trekta ya mkono ambayo hutumia lita mbili na nusu za mafuta kulima shamba la ekari moja, jambo anbalo hupunguza gharama kwani unapolima kwa kutumia treka ekari moja hugharimu kati ya Sh. 30,000 na 50,000.

Aliwataka wakuliwa na wanaotaka kuingia kwenye kilimo, kuwa na utaratibu wa kuwatembelea wakulima wanaotumia teknolojia ili kujifunza na kuboresha kilimo.

Alisema kuwa mpango wa serikali wa kuwezesha vijana kuingia kwenye kilimo utakuwa na manufaa makubwa kama watakuwa na utayari.

"Tunatakiwa kuhakikisha vijana wanaelimishwa ili wafahamu kilimo ni nini, nina amini kilimo cha teknolojia kitawavutia vijana wengi," alisema.





# Mgodi matatani kutiririsha sumu kwenye vyanzo vya maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa siku 14 kwa wamiliki wa Mgodi wa Dhahabu wa Sunshine ulioko wilayani Chunya mkoani Mbeya, kujieleza kutokana na kuchafua mazingira kwa kutiririsha maji yenye sumu kwenye vyanzo vya maji.

Maofisa mbalimbali wa NEMC kutoka makao makuu na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walifanya ziara ya kushtukiza kwenye mgodi huo mwishoni mwa wiki kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa sheria mbalimbali za uhifadhi wa mazingira ambapo walibaini baadhi ya dosari.

Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samwel Gwamaka, alisema katika uchunguzi wa awali walibaini kwamba kwenye eneo la mgodi huo kuna mabwawa mawili ya maji taka - moja lina kibali na lingine halina licha ya kwamba yote yanatumika.

Alisema mabwawa hayo hayajadhibitiwa vizuri, hali ambayo inahatarisha maisha ya wakazi wa maeneo jirani kutokana na mabwawa hayo kutiririsha maji yenye sumu kwenda kwenye vyazo vya maji vilivyoko kwenye eneo hilo.

Alisema walipofika kwenye eneo hilo, hawakuwakuta wahusika halisi na badala yake waliwakuta baadhi ya watu wenye asili ya Bara la Asia ambao hawawezi kujieleza kwa Kiswahili ama Kiingereza (walikuwa wanazungumza lugha ya Kichina tu) na hivyo ikawa vigumu kupata maelezo.

"Tumeamua kuchukua hatua ambapo kuanzia sasa eneo hili linadhibitiwa, hakuna shughuli zinazoruhusiwa kuendelea kufanyika za uchenjuaji, lakini pia wahusika wanatakiwa waje Dodoma kujieleza sababu za kutiririsha maji haya yenye sumu bila kutibu," aliagiza Dk. Gwamaka.

Aliwataka wamiliki wa mgodi huo kwenda na nyaraka mbalimbali kikiwamo cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira (EIA), vibali vya kumwaga maji pamoja na masharti waliyopewa wakati wa kuanza uzalishaji ili kujiridhisha.

Dk. Gwamaka alisema mamlaka hiyo itachukua hatua zaidi ikiwamo kuinyang'anya kampuni hiyo cheti cha mazingira, hali itakayoifanya kampuni hiyo kutoruhusiwa kufanya shughuli za uchimbaji kama inavyofanya sasa.

Alisema kwa mujibu wa sheria, mamlaka hiyo inatakiwa kumshauri Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kufuta cheti cha mazingira kwa taasisi yoyote.

Katika hatua nyingine, Dk. Gwamaka alisema kampuni hiyo imesitisha shughuli za uchenjuaji kwenye moja ya maeneo hayo kwa zaidi ya miaka mitatu bila kutoa taarifa kwenye mamlaka hiyo kuhusu udhibiti wa mazingira, jambo ambalo alisema ni kinyume cha sheria.

Meneja wa NEMC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Glory Kombe, alisema wamekuwa wakikabiliana na matatizo mbalimbali ya kimazingira ambayo yamekuwa yakifanywa na wananchi.

Alisema tatizo kubwa ambalo wamekuwa wakikabiliana nalo ni uchafuzi wa vyanzo vya maji ambao umekuwa ukifanywa na wananchi kwa njia mbalimbali ikiwamo shughuli za kilimo, ufugaji na uchimbaji wa madini.

Alisema kwenye Wilaya ya Mbarali wamekuwa wanakabiliana na wananchi wanaochepusha maji bila kuwa na vibali kwa ajili ya shughuli za kilimo.

"Tumekuwa tukishirikiana na taasisi mbalimbali kukabiliana na matatizo haya, kuna wananchi wamekuwa wakiingia kwenye maeneo ya hifadhi na kuanzisha shughuli za kilimo, wengine wanachepusha maji bila vibali, tumekuwa tukiharibu miundombinu yao na kuruhusu maji kwenda kwenye mkondo," alisema Glory.

## Barabara ya TANZAM kuwa ya njia nne

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

TATIZO la ufinyu wa barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) hasa katikati ya Jiji la Mbeya linaelekea kupatiwa ufumbuzi kwa kupanuliwa na kufanywa kuwa ya njia nne.

Tatizo hilo limekuwa likisababisha msongamano wa magari na ajali za mara kwa mara na wakati mwingine kusababisha mawasiliano kukatika inapotokea ajali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwaambia waandishi wa habari juzi jijini hapa kuwa mkataba wa upanuzi wa barabara hiyo utatiwa saini kesho kwenye eneo la Kabwe jijini. Alisema barabara hiyo itapanuliwa umbali wa Km. 29 kuanzia Nsalaga jijini Mbeya mpaka Ifisi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kwamba gharama ya mradi na jina la mkandarasi vitafahamika wakati wa kutia saini mkataba.

"Mkataba huu utakuwa baina ya Wakala wa Barabara (TANROADS) na mkandarasi, lakini utiaji saini huo utashuhudiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa," alisema Homera.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mbeya, Matali Masige, alisema maandalizi yote kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo yamekamilika ikiwamo uondoaji wa baadhi ya miundombinu iliyomo kando ya barabara.

Alisema kwenye barabara hiyo ni maeneo machache ambayo serikali italazimika kuwalipa wananchi fidia kutokana na wengi kujenga kwa kuzingatia sheria za hifadhi ya barabara.



Waziri wa Maji, Juma Aweso, akishirikiana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Maryprisca Mahundi, kukata utepe na kufunga nyaraka mbalimbali za mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Maji wa Chanzo cha Mto Kiwira mwishoni mwa wiki kabla ya mkataba huo kusainiwa baina ya maofisa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya- WSSA) na mkandarasi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Suluhisho tatizo la maji Mbeya na Songwe lanukia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTEKELEZAJI wa Mradi wa Maji wa Chanzo cha Mto Kiwira ambao unatajwa kuwa suluhisho la tatizo la maji kwenye mikoa ya Mbeya na Songwe, umeanza baada ya mkataba wa ujenzi wake kutiwa saini.

Mkataba huo ulitiwa saini juzi kati ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) na Kampuni ya China Railway Construction Enginering Group na kushuhudiwa na maofisa mbalimbali wa serikali.

Baadhi ya maofisa wa serikali walioshuhudia utiaji wa saini wa mkataba huo ni Waziri wa Maji, Juma Aweso, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, wabunge wa Mkoa wa Mbeya na viongozi wengine wa mkoa huo.

Akizungumza kabla ya kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange alisema mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbalimbali na kwamba kwa awamu ya kwanza utakuwa wa kuhudumia halmashauri mbili za mkoa huo ambazo ni Mbeya Jiji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema awamu ya kwanza itatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 117 ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kwamba awamu zingine zitafuata baada ya kukamilika ya kwanza, ikiwa ni mahususi kutoa huduma kwa maeneo mengine.

Alisema mradi huo pia utatoa huduma wilaya za Mbarali na Chunya kwa Mkoa wa Mbeya na miji mbalimbali ya Mkoa wa Songwe ukiwamo wa Tunduma ambao uko mpakani mwa Tanzania na Zambia.

"Mradi huu utakuwa ndio suluhisho la tatizo la maji kwenye jiji letu, kwa sasa tunakabiliwa na tatizo la upungufu wa maji kutokana na uwezo mdogo wa uzalishaji dhidi ya mahitaji.

"Kwa sasa uzalishaji ni lita za ujazo milioni 66.5 kwa siku wakati mahitaji ni lita milioni 90," alibainisha Kayange.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini, alisema mradi huo utamaliza tatizo la maji kwa Jiji la Mbeya ambalo kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji ni tatizo kwenye baadhi ya maeneo.

"Tunaishukuru sana serikali kwa mradi huu, tunaamini kwamba fedha zitatoka kwa wakati na mradi utakamilika mapema ili sasa wananchi waendelee kupata huduma bila matatizo," alisema Dk. Tulia.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo aliwataka viongozi wa serikali kusimamia mradi huo ili utekelezwe kwa viwango vinavyotakiwa na uwahudumie wananchi kwa muda mrefu zaidi.

Waziri wa Maji, Aweso, alisema fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao ni ahadi ya serikali zipo na utatekelezwa kwa fedha za ndani.

Alisema kuwa yeye kwa kushirikiana na Naibu Waziri wa Maji na watendaji mbalimbali wa wizara watahakikisha wanasimamia kwa karibu mradi huo ili ukamilike kwa wakati na kuanza kuwanufaisha wananchi.

# Mwinyi asifu mchango timu ya madaktari Kuwait tiba ya moyo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema timu ya madaktari bingwa wa moyo waliopo nchini wakitokea Kuwait inatoa mchango mkubwa kwa serikali katika kuwatumikia wananchi.

Amesema kuwapo kwa timu hiyo kumeongeza nguvu za kiutendaji kwenye hospitali walizofikia madaktari hao ukiwa ni mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar mwishoni mwa alipozungumza na timu hiyo iliyoongozwa na mwenyeji wao, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui.

Alisema tatizo la moyo bado linaendelea kuwasumbua wananchi wa Zanzibar na kueleza kuwa timu hiyo imekuja kutoa mchango zaidi kwa watoto wanaosumbuliwa na matatizo ya moyo.

Alisema bado kuna watoto wengi wanaokabiliwa na tatizo hilo, hivyo imani yake kuwa timu ya madaktari itatoa mchango mkubwa katia matibabu ya watoto wengi wakiwa nchini.

Alisema serikali imekuwa inatumia gharama kubwa ya matibabu ya moyo kwa kuwasafirisha wagonjwa kwenda nje ya nchi na kueleza kuwa mbali ya gharama za tiketi na matibabu ambazo wagonjwa na familia zao wanagharimia, serikali pia inabeba mzigo mkubwa kugharamia matibabu hayo.

Alisema serikali ina lengo la kutoa huduma zote nchini na kwamba magonjwa yote yanatibiwa ndani ya nchini bila kutumia gharama kubwa nje ya nchi na ndio maana imejenga hospitali za kisasa kutoa wepesi kwa wananchi wake. Dk. Mwinyi aliiahidi timu ya madaktari hao kushirikiana nao kwa kipindi chote watakachokuwapo nchini.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliishukuru timu ya madaktari hao kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali na kukubali kujitoa kuongeza nguvu kuimarisha Sekta ya Afya nchini.

Alisema timu ya madaktari hao kushirikiana na madaktari wenyeji wa Hospitali ya Mnazimmoja, wamefanikiwa kuwahudumia watoto 33 waliokuwa wakisumbuliwa na matatizo ya moyo, 30 kati yao walitibiwa na kuruhusiwa kurejea majumbani mwao na watatu wanaendelea na matibabu hospitalini huko.

Mmoja wa madaktari hao, Dk. Fesal Al - Said, alishukuru Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya kwa mapokezi yao na ushirikiano inaowapatia tangu siku walipotua nchini.

Alisema lengo la ujio wao Zanzibar ni kutoa ushirikiano kwenye kutatua matatizo yanayowakabili watoto, hasa matatizo ya moyo.




Mratibu wa Wanawake na Watoto, Shehia ya Fuoni Uwandani, Husna John, akichangia katika mkutano wa utowaji elimu ya sheria kwa wananchi wa Fuoni iliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili kupunguza vitendo vya kihalifu Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mradi mpya wa mamilioni walenga kuongeza ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkazi wa Benki ya Dunia, Nathan Balete, amesema wamefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika uimarishaji wa Sekta ya Elimu, yakiwamo maboresho ya mitaala.

Balete aliyasema hayo juzi wakati wa utiaji saini wa mradi wa miaka sita wa kuimarisha ubora wa elimu ya Zanzibar ambao unatarajiwa kugharimu dola za Marekani milioni 50.

Alisema Benki ya Dunia imeridhishwa na mradi uliomalizika wa utekelezaji wa kuimarisha miundombinu ya vifaa vya maabara na majengo ambao umejenga vituo vya sayansi 20 kwa lengo la kuongeza ufaulu katika masomo hayo.

Alisema Benki ya Dunia inafahamu miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni uimarishaji wa Sekta ya Elimu kwa kujenga miundombinu ya kisasa ya shule za ghorofa.

"Benki ya Dunia imeamua kutekeleza mradi wa uimarishaji ubora wa Sekta ya Elimu ambao utahusisha mambo mengi ikiwamo ubora wa elimu inayotolewa kwa kuwapatia mafunzo walimu," alisema.

Akizungumza baada ya utiaji saini wa utekelezaji wa mradi huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya aliipongeza Benki ya Dunia kwa kuiamini Zanzibar katika mipango yake ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano, barabara na utalii.

Kuhusu Sekta ya Elimu, Dk. Saada alisema serikali inaendelea na juhudi zake ikiwamo ujenzi wa shule za ghorofa Unguja na Pemba ambazo zitapunguza msongamano wa wanafunzi.

Alisema serikali ilitenga jumla ya Sh. bilioni 36 ambazo zilikwenda katika Sekta ya Elimu kutekeleza ujenzi wa shule mpya za ghorofa na kuzifanyia ukarabati shule kongwe.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, akifafanua utekelezaji wa mradi huo, alisema utahusisha kuwapatia walimu mafunzo kuhusu utendaji wa majukumu yao kufundisha wanafunzi kwa lengo la kuongeza ufaulu.

# Wakili: Tusiliachie Jeshi la Polisi pekee kuuzuia uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUKUMU la kuzuia vitendo vya kihalifu na uovu kwenye jamii linapaswa kufanywa na kila mtu kwenye eneo lake badala ya kuliachia Jeshi la Polisi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Hamisa Mmanga, alitoa kauli hiyo jana huko Fuoni Mkoa wa Mjini Magharibi wakati akiwasilisha mada katika ziara za kutoa elimu ya kisheria kwa jamii, ikiwa ni mwendelezo wa shamrashamra za Wiki ya Sheria Zanzibar ambayo kilele chake ni leo.

Alisema kushamiri kwa maovu katika jamii kama biashara na matumizi ya dawa za kulevya, udhalilishaji na migogoro ya ardhi huchangiwa kwa kiasi kikubwa na tabia ya muhali iliyojengeka kwa watu wengi na hivyo kushindwa kuwafichua watendaji wa maovu hayo katika jamii.

Alisema ni vyema inapotokea ishara tu ya jambo lolote ambalo ni kinyume cha sheria, wananchi watoe taarifa badala ya kukaa kimya kwa kuogopa kuonekana wabaya kwa watendaji wa makosa hayo. "Chukulia mfano mtaani kwenu wamekuja watu wasioeleweka, wakaanza kuvuta bangi au dawa yoyote, wewe ukakaa kimya, au mwanafamilia ametenda kosa ukaendelea kukaa kimya, tambua kuwa unatengeneza mazingira ya kufanyika makosa zaidi," alisema.

Wananchi waliohudhuria mkutano huo walikuwa na shauku ya kusikia hatua zinazochukuliwa kupambana na dawa za kulevya pamoja na matendo ya udhalilishaji ambayo yanawakosesha amani wakazi wa Shehia ya Fuoni.

Mmoja wa wakazi hao, Salma Ali alitaka kujua sababu za vijana wadogo kukamatwa kutokana na kuwa wasambazaji na watumiaji dawa za kulevya ilhali wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya wanafahamika bila kuchukuliwa hatua.

Alisema wananchi wengi wana hamu ya kuona wafanyabiashara wakubwa wa dawa ya kulevya wanaotoa dawa hizo nje ya nchi, wanatiwa hatiani na kupewa adhabu badala ya kila siku kuonekana vijana wadogo wanaotumia dawa hizo ndio wanaotiwa hatiani. Akijibu swali hilo, Wakili kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Issa Ahmed, alisema hawana taarifa ya wafanyabiashara hao wakubwa wanaodaiwa kufanya biashara hiyo.

Alisema kama kuna mwananchi yeyote mwenye taarifa ya wafanyabiashara Wakubwa na wadogo, anapaswa kulijulisha Jeshi la Polisi ili lifanye kazi yake.

Mrakibu wa Polisi Kituo cha Fuoni, Denis Tumbo, alisema jeshi hilo lipo tayari muda wote na hivyo aliwashauri wananchi hao kuwa karibu nalo ili kufanya kazi ya kulinda usalama wa wananchi wote.

Ziara hiyo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ikilenga kuwafahamisha wananchi sheria kama njia mojawapo ya kusaidia kupunguza migogoro ikiwamo ya ardhi, vitendo vya udhalilishaji, dawa za kulevya na uhalifu kwenye jamii.

# Bwawa la Nyerere kusaidia mradi wa maji kuja Dar

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inatarajia kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Rufiji utakaohudumia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Mradi huo utakaozalisha lita milioni 750 kwa siku ni wa manufaa makubwa kwa kuwa utawezesha maji ya Mto Rufiji kutumika kuzalishia maji kwa ajili ya mikoa hiyo miwili yenye biashara na viwanda vingi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya DAWASA, Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyange, wakati wa ziara ya bodi ya mamlaka hiyo iliyolenga kukagua chanzo cha mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Julius Nyerere (JNHPP).

"Tumefurahishwa sana na utekelezaji wa mradi huu na tunaipongeza sana serikali kwa kusimamia ukamilishaji wa mradi huu utakaoleta tija kubwa kwa taifa," alisema na kuongeza:

"Kasi ya ukamilishaji wa mradi huu ni kubwa na nipende kusema kuwa kupitia mradi huu DAWASA itakwenda kutekeleza mradi wa maji Rufiji utakaohudumia Mkoa wa Pwani na sehemu ya Mkoa wa Dar es Salaam," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Cyprian Luhemeja alisema utekelezaji wa mradi wa maji Rufiji utaenda kuongeza na kuimarisha kiwango cha upatikanaji wa maji katika eneo la kihuduma la DAWASA.

"Ziara hii ya Bodi ya Wakurugenzi imekuja kuona chanzo cha maji cha mradi wa Rufiji ambao ni Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao upo katika hatua za mwisho za utekelezaji wake," alisema Luhemeja.

Alisema kwa sasa mamlaka inazalisha lita milioni 590 wakati mahitaji yakiwa lita milioni 540, hivyo kupitia mradi wa maji Rufiji wanatarajia kuzalisha lita milioni 750 zitakazosaidia kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa Mkoa wa Pwani pamoja na wilaya jirani.


"Utekelezaji wa mradi wa maji Rufiji upo katika hatua ya kufanya usanifu na kuandaa michoro ya mradi baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu utekelezaji utafanyika mara moja," alisema.

Alisema mtambo wa uzalishaji maji Rufiji unatarajiwa kujengwa katika kijiji cha Mloka Wilayani Rufiji kijiji kilicho jirani na mradi wa JNHPP.

Mhandisi mkazi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la JNHPP, Lutengano Mwandambo, alisema utekelezaji wa mradi umefika asilimia 81 huku kazi ya kujaza maji kwenye bwawa ikiendelea na kufikia kina cha mita 131.2 kutoka usawa wa bahari.

"Kazi ya kujaza bwawa ilianza rasmi mwezi Desemba 2022 kwa kina cha mita 74.8, hadi sasa tumefikia kina cha mita 131.2 kutoka usawa wa bahari na matarajio yetu ni kufikisha kina chenye mita 163," alifafanua.

Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere ulianza kutekelezwa mwaka 2018 kwa lengo la kuzalisha umeme Megawati 2115 na unatekelezwa na kampuni ya Arab Contractor na Elsewedy Eletric kwa gharama ya Sh. trilioni 6.5.




Wakala wa Tigo Pesa Saba General Enterprises Limited ambaye ni wakala aliyefikisha lengo la miamala kiufasaha akipokea mfano wa hundi yenye kiasi cha Sh. milioni moja kwa Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Angelica Pesha (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti, Uhusiano na Serikali Slyvia Balwire (kulia). Mwingine ni Mkuu wa Kitengo cha kusimamia Mawakala wa Tigo Pesa, Innocent Mosha (kushoto). P**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji kuku wahoji ubora chakula

**Na Mary Geofrey**

WAFUGAJI wa kuku wamewataka watengenezaji wa chakula cha mifugo kufanya utafiti kujua ubora wa bidhaa wanazouza.

Mmoja wa wafugaji hao, Sostenes Vicent, mkazi wa Kibaha, alitoa wito huo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa semina ya wafugaji na wakulima kuhusu matumizi ya mbolea na chakula cha mifugo yaliyoandaliwa na Kampuni ya Shama Mills inayozalisha na kuuza bidhaa hizo.

Alisema watengenezaji wa vyakula vya mifugo ikiwamo kuku, wamekuwa wakizalisha bidhaa zilizo chini ya kiwango na kuathiri ukuaji na kupata uzito pungufu.

"Unanunua chakula cha kulisha kuku gharama kubwa ukitarajia baada ya wiki moja kuku atakuwa uzito fulani, lakini chakula kinaisha kuku hana ule uzito, hii inatudhoofisha wafugaji kwa sababu tunashindwa kufikia malengo yetu ya kuuza bidhaa zenye ubora na kupata faida," alisisitiza.

Mfugaji Najma Ghani alisema vyakula vya mifugo vipo chini ya kiwango na hali hiyo inasababisha kuharibu soko na biashara kwa ujumla.

"Tumekuja kwenye mafunzo hapa tumepewa elimu ya namna ya kufuga na kuzingatia milo kamili ya mifugo, kabla ya kuiuza lakini je kama bidhaa zipo chini ya kiwango tunafikiaje lengo?" alihoji na kuongeza:

"Tunaishukuru kampuni ya Shama Mills ambao wamekuja na bidhaa hizi ambazo kwa maelezo yao, zinakidhi viwango vinavyokubalika, ninaamini tutakwenda kufuga kisasa na kupata faida."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Shama Mills, Mohamed Nasir, aliwataka wafugaji hao kuzingatia milo tatu ya kuku wanaowafuga wa vifaranga, ukuaji na hatua ya kuchinjwa.

Alisema mbali na kuwa wanatoa bidhaa zenye ubora unaokubalika nchini, wafugaji wanatakiwa kuzingatia taratibu ambazo zitawafanya wapate faida ikiwamo kuuza kuku wa kuanzia wiki nne.

# Madai uvamizi 'panya road' yazua taharuki

**Na Elizabeth Zaya**

MAENEO ya Bunju usiku wa kuamkia jana yalikumbwa na taharuki baada ya kudaiwa kuwapo kikundi cha vijana wahalifu wa mitaani, maarufu panya road kilichokuwa kinapanga kuvamia maeneo hayo.

Taharuki hiyo iliibuka ikiwa ni siku chache tangu wakazi wa eneo la Bunju B, Mtaa wa Idara ya Maji kuvamiwa na watu waliodaiwa kuwa ni kikundi hicho na kujeruhi watu kadhaa.

Taharuki hiyo ilizuka kuanzia majira ya saa moja jioni hadi saa tatu usiku kwa watu waliokuwa wakihamasishana kuondoka kwenye maeneo ya barabarani wakidai tayari kundi hilo limeanza kuvamia baadhi ya maeneo ya biashara na starehe wakianzia Bunju Usalama.

Kadri watu walivyozidi kusambaza taarifa hizo ndivyo taharuki ilivyozidi kutawala, watu wakikimbia kurejea nyumbani na kufunga maduka yao.

Sio maduka pekee, bali familia zililazimika kujifungia ndani ya nyumba zao na ukimya ukatawala muda huo. Sehemu za starehe ikiwamo baa, watu walilazimika kuondoka.

Nipashe ilipozungumza na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema tarahuki hizo zilizushwa na kikundi cha vijana ambao walitoka kuangalia mpira kati ya Simba na Horoya ambao walikuwa wanafanya utani kwamba kuna panya road.

"Sisi Jeshi la Polisi tulikuwapo Bunju, hakukuwa na panya road. Kulikuwa tu na kundi la vijana ambao baada ya kutoka kuangalia mechi ya Simba na Horoya, walikuwa wakifanya utani na hivyo kusababisha hizo taharuki.

"Baada ya kutokea kwa taharuki hiyo, nimepigiwa simu na watu wengi sana na wengine ni waheshimiwa lakini tulipowabana zaidi tukiwaambia sisi tuko eneo la tukio, wakasema wao wako nje ya Dar es Salaam lakini wameambiwa na familia zao kwamba kuna panya road wamevamia," alisema.

Kamanda huyo aliwataka watu wakaache kuzua taharuki za namna hiyo na kusababisha shida kwa wananchi.

"Ni kweli taharuki ilikuwa kubwa na baadhi ya maduka yalifungwa, lakini hakukuwa na tishio lolote, ni vyema watu wakaacha tabia hii ya kuzua taharuki kwa mambo ambayo ni ya hatari," alisema Murilo.

Usiku wa kuamkia Februari 10 mwaka huu, kundi linalodhaniwa kuwa ni la panya road lenye zaidi ya watu wanane, lilivamia makazi ya watu eneo la Bunju B, Mtaa wa Idara ya Maji saa nane usiku.

Kwa mujibu wa Kamanda Murilo, pamoja na kujeruhi, pia walisababisha uharibifu ikiwamo kupasua runinga kwa watu walioshindwa kuwapatia fedha.

## HABARI KIMATAIFA

# Waliokufa kwa tetemeko wafikia 28,000

**INSTANBUL,** Uturuki

IDADI ya watu waliokufa kutokana na tetemeko la ardhi lililoikumba Uturuki na Syria siku kadhaa zilizopita imetajwa kufikia 28,000 huku jitihada za uokoaji kutafuta watu waliokwama chini ya vifusi vya nyumba zilizoporomoka ikiendelea.

Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, akiwa katika jimbo la Diyarbakir lililokumbwa na maafa hayo, alisema nchini humo watu takribani 21,000 wamekufa na wengine zaidi ya 80,000 wamejeruhiwa.

Alibainisha kuwa mpaka jana watu takribani 102,000 walishahamishwa na kupelekwa sehemu nyingine baada ya makaazi yao kuharibiwa na kwamba vikosi vya waokoaji takribani 166,000 vikiwamo vya kutoka mataifa mbalimbali vinaendelea na juhudi za uokoaji.

**Maofisa nchini Uturuki wanasema vibali 113 vya kukamatwa kwa waliohusika na ujenzi wa majengo yaliyoporomoka wakati wa tetemeko la ardhi vimetolewa.**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus pamoja na Mratibu wa Misaada wa Umoja wa Mataifa, Martin Griffiths, wamewasili kwenye mji wa Allepo nchini Syria ambako watu zaidi ya milioni tano wameathiriwa na tetemeko la ardhi.

Inaelezwa kuwa WHO limepeleka tani 35 za dawa muhimu na msaada mwingine unatarajiwa kupelekwa katika siku mbili zijazo.

Watu kadhaa wameokolewa siku tano baada ya maafa kutokea na kwamba msichana mwenye umri wa miaka minne alikuwa miongoni mwa waliokolewa kwenye mji wa Gaziantep nchini Uturuki, baada ya kuwa chini ya kifusi kwa muda wa saa 130.

Inaelezwa kuwa vikosi vya uokozi vya Ujerumani na Austria vimesimamisha shughuli za kuwatafuta watu kwenye jimbo la Hatay la nchini Uturuki kutokana na sababu za kiusalama, ikidaiwa kuwa kuna taarifa juu ya kuzuka mivutano kwenye jimbo hilo na milio ya bunduki ilisikika.

Rais Tayyip Erdogan alisema idara husika zilipaswa kufanya haraka ili kuwasaida waathirika, akiahidi kuanza kazi haraka kwa ajili ya ujenzi mpya, lakini amewaonya wahalifu wanaopora mali za watu wakati huu wa maafa.

Misaada pia iliwasili nchini Syria licha ya kuwa ya kiwango cha chini kutokana na athari za vita vya muda mrefu na kwamba shughuli za kupeleka misaada hiyo zinatatizika hata baada ya serikali ya nchi hiyo kusema kwamba itaruhusu misaada kupelekwa.

Mkuu wa kitengo cha misaada cha Umoja wa Mataifa, Griffiths, alisifu juhudi zinazofanywa na Uturuki katika kuwashughulikia watu waliokumbwa na maafa ambayo hayajawahi kushuhudiwa kwa karne.

Mwendesha mashtaka wa serikali nchini Uturuki, alisema uchunguzi utafanywa juu ya majengo yaliyosambaratika ili kubainisha iwapo palikuwapo hitilafu katika ujenzi.

Aidha, maofisa nchini Uturuki wanasema vibali 113 vya kukamatwa kwa waliohusika na ujenzi wa majengo yaliyoporomoka wakati wa tetemeko la ardhi vimetolewa.

Hata hivyo kwa mujibu wa taarifa, polisi wa nchini Uturuki tayari wamewaweka chini ya ulinzi watu takribani 12, wakiwamo makandarasi wa ujenzi, akiwamo mmoja aliyekamatwa wakati alipokuwa anasubiri kupanda ndege mjini Istanbul. **DW/BBC**

## Wanawake Russia wakimbilia Argentina

**MOSCOW,** Russia

ZAIDI ya wanawake 5,000 wajawazito wa nchini Russia wametajwa kukimbilia nchini Argentina katika miezi ya hivi karibuni, ikiwamo 33 waliosafiri kwa ndege moja mwishoni mwa juma lililopita.

Kwa mujibu wa taarifa ya wakala wa kitaifa wa uhamiaji Carignano, wanawake waliofika nchini Argentina siku za hivi karibuni wote walikuwa katika wiki za mwisho za ujauzito.

Inaaminika kuwa wanawake hao wanataka kuhakikisha watoto wao wanazaliwa nchini Argentina ili kupata uraia wa taifa hilo.

Hata hivyo, inaelezwa kwamba idadi ya waliowasili nchini humo imeongezeka hivi karibuni, huku vyombo vya habari vya ndani vikiashiria hatua hiyo imetokana na vita vya Ukraine.

Vile vile, inaelezwa kuwa wanawake hao wa Russia hapo awali walidai kuwa walikuwa wakitembelea Argentina kama watalii.

"Tulibaini kwamba hawakuja hapa kufanya shughuli za utalii, walikubali wenyewe," alisema Carignano.

Alisema wanawake wa Russia walitaka watoto wao wawe na uraia wa Argentina kwa sababu ilitoa uhuru zaidi kuliko pasipoti ya Russia.

"Tatizo ni kwamba wanakuja Argentina, kuwasajili watoto wao kama Waargetina na kuondoka. Pasipoti yetu ni salama kote duniani. Inawaruhusu waliyo nayo kuingia nchi 171 bila visa," alisema Carignano.

Aliongeza kuwa na mtoto Muargentina pia kunasaidia kuharakisha mchakato wa wazazi kupata uraia, na kwamba kwa sasa Warussia wanaweza kusafiri bila visa katika nchi 87 pekee. **BBC**




Waandamanaji wakionekana katika mji wa Toulouse, Kusini mwa Ufaransa, juzi. **PICHA: AFP**

## Wapinga marekebisha mfumo pensheni

**PARIS,** Ufaransa

WANANCHI wamefanya maandamano kwa siku nne mfululizo nchini Ufaransa ili kupinga mipango ya Rais wa taifa hilo Emmanuel Macron ya kurekebisha mfumo wa pensheni wa nchi hiyo.

Inaelezwa kuwa maelfu ya watu walitarajiwa kuandamana jana katika miji ya Paris, Nice, Marseille, Toulouse na Nantes kwa matumaini ya kuendeleza shinikizo kwa serikali kurejea.

Maandamano hayo yaliwavutia vijana na wengine waliopinga mapendekezo ya pensheni ambao hawakuweza kuhudhuria siku tatu za awali wakati maandamano yalipofanyika siku za kazi.

Hata hivyo, mgomo wa wafanyakazi wa reli unaelezwa kuwa haukuambatana na maandamano hayo na kuruhusu treni za Paris Metro kufanya kazi Jumamosi.

Vile vile, inaelezwa kuwa mgomo usiotarajiwa wa wafanyakazi wa kuongoza ndege uliripotiwa mwishoni mwa wiki na kwamba nusu ya safari za ndege kuingia na kutoka katika uwanja wa pili kwa ukubwa wa Paris, Orly, ziliahirishwa. **VOA**

## Wanajeshi washambuliwa na wanamgambo Somaliland

**SOMALILAND,** Somalia

WANAJESHI wa Jimbo la Somaliland nchini Somalia, wameshambuliwa na watu wenye silaha, licha ya kuwapo kwa maelewano ya kusitisha mapigano makali ambayo yamekuwa yakiendelea wiki iliyopita.

Inaelezwa kuwa mashambulio hayo yaliyotekelezwa mwishoni mwa juma lililopita, yalijiri baada ya Waziri wa Ulinzi katika jimbo hilo Abdiqani Mahamoud, kutangaza makubaliano ya kuacha makabiliano bila masharti yoyote.

Licha ya shambulio hilo, waziri huyo, alisema jeshi la Somaliland lilifanikiwa kujilinda na kwamba hali ya tahadhari inashuhudiwa katika kambi yao ya Las Anod.

Inabainishwa kuwa wiki iliyopita watu 20 waliuawa baada ya mapigano kati ya wanajeshi wa jimbo hilo na kundi lenye silaha katika mji unaowaniwa wa Las Anod, unaopambaniwa na uongozi wa jimbo hilo na jimbo lingine la Puntland.

Hata hivyo Somaliland, ilijitangazia uhuru wake tangu 1991 kutoka uongozi wa Mogadishu, lakini haijawahi kutambuliwa kimataifa, licha ya kuendelea kushuhuhudia uthabiti hasa wa kisiasa na usalama kwa kipindi kirefu nchini humo. **RFI**

# DODOMA JIJI FC YAONGOZA KUZAWADIWA PENALTI, KUKOSA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Dodoma Jiji imeweka rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kupata penalti nyingi kuliko timu zingine, lakini imeongoza pia kwa kukosa.

Dodoma Jiji inayoshikilia nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 24 kwa mechi 22, ilizocheza imefanikiwa kuzawadiwa penalti sita mpaka sasa, lakini imepata moja tu na kukosa tano zilizobaki, ikiwa ni rekodi ya aina yake.

**Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, timu inayofuata kwa kutengeneza penalti nyingi kwenye ligi ni Geita Gold, Prisons na Singida Big Stars, kila timu ikipata penalti nne, lakini kila moja ikizitua kivyake.**

Geita Gold na Prisons imepachika penalti zao zote nne kila mmoja kwenye kamba, lakini Singida Big Stars ikikosa moja.

Timu zilizoshika nafasi ya tatu kwa kupata penalti nyingi kwenye ligi ni Simba, Yanga, KMC na Ruvu Shooting kila moja ikiwa imepata tatu.

Simba na KMC zimeonekana kutumia vema penalti zao kwa kupachika ndani ya nyavu zote tatu, lakini Yanga na Ruvu Shooting kila moja ikifunga mbili na moja ikiota mbawa.

Takwimu hizo ni mpaka raundi ya 22 ya Ligi Kuu ya Tanzania ambayo mpaka sasa Yanga inaongoza ikiwa na pointi 59 na ni timu iliyoruhusu mabao machache zaidi, wavu wake ukitikiswa mara 10, ikifuatiwa na Simba yenye pointi 53, ambayo ni timu iliyofunga mabao mengi zaidi mpaka sasa ikiwa imepachika mabao 54.

Geita Gold mpaka sasa ndiyo timu yenye sare nyingi zaidi ikiwa nazo 10 kwa mechi 22 ilizocheza, Ruvu Shooting ikiwa ni timu iliyopoteza mechi nyingi zaidi hadi sasa, ikiwa imeshapoteza mechi 13.

**JEZI...**




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Mauzo wa Benki ya Stanbic, Emmanuel Mahodanga (kushoto), akikabidhi jezi za michezo zenye thamani ya Sh. milioni tano kwa ajili ya wanafunzi wa Shule za Sekondari Chinangali na Nzugun zilizoko Dodoma kwa Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Jamal Ngalya (kulia). Msaada huo unalenga kuhamasisha wanafunzi kushiriki katika shughuli za michezo na kuunga mkono juhudi za serikali za kukuza michezo shuleni. Kushoto ni Meneja wa Tawi la Benki ya Stanbic Dodoma, Joan Mbise. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mukala amtishia 'nyau' Kidunda*



**Na Saada Akida**

MPINZANI wa bondia Seleman Kidunda, Patric Mukala raia wa DR Congo (pichani), amemtumia salamu za kumtisha 'nyau' mpinzani wake baada ya kumwambia anakuja nchini kwa kazi moja ya kuhakikisha anamchapa vibaya katika pambano lao linalotarajia kupigwa Februari 24, mwaka huu katika Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Mukala na Kidunda watapanda ulingoni kwenye pambano hilo kuwania mkanda wa Ubingwa wa Afrika ABU sawa na Mtanzania mwengine, Tony Rashid, atakayetetea mkanda wake wake wa ABU dhidi ya Sabelo Ngabinyana raia wa Afrika Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, Mukala alisema kazi inayomleta Tanzania ni moja tu, kuhakikisha anafanikiwa kumchapa mpinzani wake ili kuweza kushinda mkanda wa ubingwa wa Afrika kutokana na maandalizi makubwa anayoendelea kufanya.

"Maandalizi yanaendelea vizuri tangu Desemba mwaka jana, naamini litakuwa pambano zuri kwangu kwa sababu nataka nimweleze Kidunda kwamba mimi si Katompa [Tshimanga], anatakiwa ajiandae maana nakuja Tanzania kwa sababu yake," alisema Mukala.

Alisema amekuwa akimfuatilia mpinzani wake katika mapambano mbalimbali ikiwamo la mwaka jana alipocheza na Katompa, hivyo anajua ubora na madhaifu ya Kidunda anapokuwa ulingoni.

"Kidunda ni mzuri, lakini sitamani kuangalia rekodi yake ipoje na siwezi kutabiri kwamba nitamchapa kwa KO, lakini ninachomwambia ajiandae vizuri kwa sababu moto mkali unakuja mbele yake," alisema Mukala.

# Simkoko kocha mpya Ihefu FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ihefu FC ambayo kwa sasa imeanza kufanya vema kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, imemteua kocha mkongwe nchini, John Simkoko, kuwa Kocha Mkuu wa klabu hiyo, akitwaa nafasi ya Juma Mwambusi ambaye aliondoka kutokana na matatizo ya kifamilia.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana mchana, ilieleza Simkoko ambaye pia aliwahi kuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, ndiye atachukua mikoba ya Mwambusi ambapo sasa atashirikiana na kocha msaidizi ambaye alikuwa anakaimu, Zuberi Katwila.

"Rasmi, timu yetu imefikia makubaliano na Kocha John Simkoko kuwa Kocha Mkuu wa Klabu yetu ya Ihefu.

Simkoko (pichani chini) ataungana na benchi la ufundi lililopo kufanikisha malengo yetu, karibu Ihefu SC," Ilieleza taarifa rasmi ya klabu hiyo.

Kocha huyo baada ya kucheza soka, alianza rasmi kufundisha mwaka 1985 kwenye timu ya Reli ya Morogoro ambayo ilitikisa enzi hizo kwa kuzifunga timu za Simba na Yanga, kiasi cha kupachikwa jina la 'Kiboko ya Vigogo', Tumbaku pia ya huko na Mtibwa Sugar.

Mara ya mwisho alionekana kwenye benchi la KMC 2020 akiifundisha timu hiyo, na sasa ameibukia Ihefu ambayo imejinasua mkiani, ikiwa inashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku jana ikicheza mechi yake ya ligi dhidi ya Singida Big Stars kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya.

Mwambusi ambaye alichukua jukumu la kuifundisha timu hiyo Septemba mwaka jana huku Katwila akirudishwa kuwa kocha msaidizi, alijiweka kando Januari mwaka huu kwa kile alichodai kushughulikia matatizo ya kifamilia.



## ZISIKUPITE

### SALAH SASA KUUZWA

KLABU ya Liverpool huenda ikakubali kuwauza wachezaji wake nyota mwishoni mwa msimu akiwamo mshambuliaji kinara rai wa Misri, Mohamed Salah, 30. ***(Football Insider)***

### KLOPP ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid imefanya mawasiliano na kocha wa Liverpool, Mjerumani Jurgen Klopp, 55, juu ya uwezekano wa kuchukua mikoba ya Mtaliano Carlo Ancelotti, 63, ili kuinoa miamba hiyo ya Hispania kuanzia msimu ujao. ***(El Nacional)***

### MATIP BEI CHEE LIVER

LIVERPOOL watakubali ofa ya wastani wa pauni milioni 15 ili kumuuza beki wao raia wa Cameroon, Joel Matip. ***(Football Insider)***

### MOUNT NA CHELSEA

BAADHI ya maofisa wa Chelsea wamechoshwa na hatua ya kiungo wao raia wa England, Mason Mount, 24, kukataa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### RASHFORD KUFUNGWA ZAIDI

KLABU ya Manchester United ipo katika mazungumzo na mshambuliaji wao kinara raia wa England, Marcus Rashford, 25, ili kuongeze mkataba. ***(GiveMeSport)***

### MILINKOVIC-SAVIC, NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inasuka mpango wa kumsajili kiungo wa klabu ya Lazio na timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, 27, ambaye ana mkataba na klabu yake hadi mwaka 2024. ***(Il Messagero, via Goal)***

### DYBALA AWINDWA UNITED

MANCHESTER United ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa klabu ya Roma na raia wa Argentina, Paulo Dybala, 29. ***(Calciomercato)***

### KESSIE AFUNGUKA SPURS

KIUNGO wa Klabu ya Barcelona na raia wa Ivory Coast, Franck Kessie, 26, alikataa kujiunga na Klabu ya Tottenham Hotspur katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Sport)***

### FELIX ATAKIWA ATLETICO

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, 23, ambaye kwa sasa yupo Chelsea kwa mkopo, ndiye mchezaji kinara atakayewindwa na Real Madrid katika dirisha la usajili la mwishoni mwa msimu kipindi cha majira ya joto. ***(Fichajes)***


### GUARDIOLA ANYATIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inahaha kumnyakua kocha wa Manchester City, Mhispania Pep Guardiola, 52. ***(El Nacional)***

### KANE HAONDOKI SPURS

NAHODHA na mshambuliaji kinara wa Timu ya Taifa ya England na Klabu ya Tottenham Hotspur, Harry Kane, 29, anatazamiwa kukataa ofa ya kujiunga na timu yoyote kubwa barani Ulaya ili kusalia Ligi Kuu England. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ALIA NA BAO LA BRENTFORD ARSENAL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema kwamba, Arsenal walistahili ushindi baada ya bao la kusawazisha la Ivan Toney kuwafanya wamalize mchezo kwa sare ya 1-1 kwenye Ligi Kuu ya England dhidi ya Brentford Jumamosi.

**Arsenal ilikosa nafasi ya kuwa mbele kwa pointi nane mbele ya Manchester City katika kilele cha msimamo ilipozuiwa na 'Nyuki' hao katika mchezo wa dabi ya London kwenye Uwanja wa Emirates.**

Leandro Trossard aliingia akitokea benchi na kufungua ukurasa wa mabao kwa bao lake la kwanza kwa klabu hiyo kipindi cha pili, lakini Toney alisawazisha kwa kichwa dakika ya 74.

**Ni la kuotea, pengine tutapata maelezo baadaye, lakini leo (juzi) hatujapata hilo...**

Na Kocha wa Arsenal, Arteta haamini kwamba bao la mshambuliaji huyo lilipaswa kutolewa.

Mhispania huyo alisema: "Nimeiangalia tu nyuma na ni ya kuotea. Pengine tutapata maelezo baadaye, lakini leo (juzi) hatujapata hilo."

Alipoulizwa kama walikuwa wameweka wazi hisia zao kwenye Ligi Kuu, alijibu: "Ndiyo, tulifanya nao mwishoni mwa mchezo na tukasema maoni yetu."

Arsenal wako mbele kwa pointi sita mbele ya City, ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Aston Villa kabla ya mpambano mkali kati ya timu mbili za juu Jumatano ijayo na Arteta aliwasifu wachezaji wake licha ya kutokuwa katika kiwango bora tena kufuatia kushindwa na Everton wikendi iliyopita.

Aliongeza: "Nadhani ni mchezo mzuri sana. Nadhani ni timu gumu sana kucheza dhidi yao. Inasikitisha, lakini hii ni Ligi Kuu.

"Nimefurahishwa na jinsi wavulana walijaribu, ni kiasi gani wanataka. Mwitikio wanapoacha pointi mbili, wako mahali pazuri."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 472,

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
EVERTON
1 | 1.49
X | 4.27
2 | 5.75

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MADRID WATWAA TAJI LA TANO KLABU BINGWA DUNIA

**RABAT,** Morocco

VINICIUS Junior na Federico Valverde kila mmoja alifunga mabao mawili wakati Real Madrid ikishinda Kombe la Dunia la Klabu la Fifa kwa mara ya tano baada ya kushinda 5-3 dhidi ya Al Hilal ya Saudi Arabia katika mchezo wa fainali Jumamosi mjini Rabat, Morocco.

Washindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Madrid walipewa nafasi kubwa zaidi dhidi ya wenzao kutoka Asia na wakawa mbele kwa mabao 2-0 ndani ya dakika 20 kwa mabao mawili ndani ya dakika tano kutoka kwa Vinicius na Valverde.

Lakini Al Hilal, timu ya kwanza kutoka Saudi Arabia kutinga fainali ya michuano hiyo, ilifanya mchezo huo kuwa mpambano baada ya kurudisha bao lililofungwa na Moussa Marega.

Madrid walipeleka moto kwa mara nyingine tena kwa mabao mengine mawili ya haraka haraka mwanzoni mwa kipindi cha pili kupitia kwa Karim Benzema aliye fiti tena na la pili kwa kiungo wa Uruguay, Valverde.

Miamba hao wa Hispania sasa imeshinda fainali zote tano walizocheza katika shindano hilo, baada ya hapo awali kushinda mataji matatu ndani ya miaka minne kati ya 2014 na 2018.

Timu iliyofuata yenye mafanikio zaidi katika mashindano ya FIFA, ambayo yalianza mwaka 2000 na yamekuwa yakifanyika kila mwaka tangu 2005, ni Barcelona wakiwa washindi mara tatu.

Timu za Ulaya sasa zimeshinda kombe hilo katika michuano 10 iliyopita ya Klabu Bingwa ya Dunia.

"Nadhani tunaimarika, kulikuwa na makosa kadhaa nyuma, lakini ubora mwingi mbele," alisema Ancelotti,



# Guardiola na mataji ya City

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema hakuna mtu anayeweza kunyang'anya mafanikio ya klabu hiyo hata kama uchunguzi unaendelea wa Ligi Kuu England kuhusu masuala yao ya kifedha.

City wameshitakiwa kwa ukiukaji wa kanuni za fedha za Ligi Kuu kutoka mwaka 2009 hadi 2018 na wanaweza kukabiliwa na kupoteza mataji matatu ya Ligi Kuu England waliyoshinda katika kipindi hicho.

City ilitoa taarifa Jumatatu ikisema: "Klabu inakaribisha mapitio ya suala hili na tume huru, ili kuzingatia bila upendeleo mwili wa kina wa ushahidi usiopingika ambao upo kuunga mkono msimamo wake."

Guardiola alisema haijalishi matokeo ya uchunguzi wa Ligi Kuu ya England ni nini, mbio za City kushinda mataji daima zitastahili kutambuliwa.

"Mwishoni, kila mara tunaondoka tukifikiria watu wengine wanafikiria nini kutuhusu. Sahau kuhusu hilo. Fikiri tulichofanya. Hakuna anayeweza kukiondoa," Guardiola alinukuliwa akisema na vyom
vya habari vya Uingere
Jumamosi.

"Nyakati mbaya tunac
doka, lakini haitabadilil
ilijengwa kutoka siku
kwanza, tulishinda sa
tunataka kutetea naf
hiyo.

"Ligi Kuu itaamua lak
najua tulishinda nini,
jinsi tulivyoshinda, kwa
dii tuliyoweka.

"Kwa jambo lililotok
mwaka 2009 au 20
sielewi ni muda gani, ha
tabadilika hata sekun
moja, ni wa kwetu, ni
kwetu kabisa, bila kuj
hukumu ni yetu."

,189,430

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/02/23 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 02. 15/02/23 | 22:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.71 | 3.24 | 2.48 |
| 03. 15/02/23 | 22:45 | Motherwell vs St Mirren | 2.36 | 3.23 | 2.93 |
| 04. 15/02/23 | 22:45 | Preston vs Luton Town | 2.53 | 3.13 | 2.73 |
| 05. 15/02/23 | 23:00 | Borussia Dortmund vs Chelsea | 2.37 | 3.37 | 2.77 |
| 06. 16/02/23 | 06:05 | Club Necaxa vs UNAM Pumas | 2.45 | 3.35 | 2.71 |
| 07. 16/02/23 | 20:45 | RB Salzburg vs Roma | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 08. 16/02/23 | 20:45 | Sporting Braga vs Fiorentina | 2.43 | 3.39 | 2.74 |
| 09. 16/02/23 | 23:00 | Sevilla FC vs PSV Eindhoven | 2.24 | 3.39 | 3.05 |
| 10. 16/02/23 | 23:00 | Sheriff Tiraspol vs Partizan | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 17/02/23 | 00:00 | Mirassol SP vs Ituano SP | 2.68 | 2.89 | 2.63 |
| 12. 17/02/23 | 03:30 | Corinthians vs Palmeiras | 3.00 | 2.75 | 2.24 |
| 13. 17/02/23 | 11:45 | Western United vs Wellington Phoenix | 2.70 | 3.23 | 2.53 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 13/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:45 | 3456 | Fajr Sepasi vs Saipa Karadj | 2.55 | 2.55 | 3.15 |
| 13:45 | 4022 | Khosheh Talaei vs Arman Gohar Sirjan | 2.24 | 2.70 | 3.54 |
| 13:45 | 5025 | Kheybar Khorramabad FC vs Vanpars | 1.77 | 2.60 | 5.40 |
| 14:00 | 2332 | Pars Jonoubi Jam vs Chooka Talesh FC | 1.64 | 3.16 | 5.80 |
| 14:00 | 3565 | Aizawl FC vs Minerva FC | 2.85 | 3.17 | 2.30 |
| 14:30 | 2083 | Psis Semarang vs Dewa United | 2.09 | 3.21 | 3.21 |
| 14:30 | 4112 | Teraktor Sazi vs Aluminium Arak | 2.09 | 2.90 | 3.62 |
| 15:00 | 3749 | Bylis Ballsh vs Partizani Tirana | 2.90 | 2.90 | 2.20 |
| 16:00 | 1911 | Al Jabalain vs Najran SC | 1.84 | 3.21 | 4.08 |
| 16:10 | 4372 | AL Ain vs Ohud Medina | 2.70 | 2.65 | 2.55 |
| 16:30 | 2972 | Kenkre FC vs Sudeva Delhi FC | 2.42 | 3.10 | 2.74 |
| 16:30 | 3686 | MES Rafsanjan vs Foolad Khuzestan | 2.38 | 2.45 | 3.67 |
| 16:30 | 3835 | Persepolis FC vs Havadar | 1.68 | 3.21 | 5.18 |
| 16:45 | 4724 | Al Fehaheel vs Al Kuwait SC | 5.61 | 3.95 | 1.50 |
| 18:00 | 1251 | Lamia vs OFI Crete | 2.81 | 3.03 | 2.57 |
| 18:00 | 1848 | Sepsi Osk vs Chindia Targoviste | 1.66 | 3.55 | 5.08 |
| 18:30 | 4951 | Manama Club vs Al Hala Muharraq | 1.69 | 3.31 | 4.87 |
| 19:00 | 3697 | Asteras Tripolis vs PAOK | 4.33 | 3.44 | 1.81 |
| 19:30 | 5520 | AEK Athens vs Levadiakos | 1.14 | 7.03 | 18.11 |
| 20:00 | 2994 | Smouha Club vs Zamalek | 3.18 | 2.88 | 2.42 |
| 20:00 | 3832 | Chojnice vs Skra Czestochowa | 1.98 | 3.36 | 3.36 |
| 20:30 | 3506 | Nancy vs Concarneau | 2.82 | 3.09 | 2.46 |
| 20:30 | 4163 | Verona vs Salernitana | 1.82 | 3.43 | 4.18 |
| 21:00 | 1925 | MTK Budapest vs Bekescsabai Elore | 1.33 | 4.67 | 7.48 |
| 21:00 | 2295 | Belenenses vs Penafiel | 2.84 | 3.11 | 2.43 |
| 21:00 | 2452 | Viktoria Koln vs RW Essen | 2.12 | 3.32 | 3.27 |
| 21:00 | 4249 | Warta Poznan vs Miedz Legnica | 1.88 | 3.22 | 3.89 |
| 21:00 | 5420 | Mafra vs Nacional Madeira | 1.99 | 3.30 | 3.57 |
| 21:00 | 5531 | Petrolul Ploiesti vs Hermanstadt | 2.66 | 2.98 | 2.71 |
| 21:30 | 1034 | Waasland Beveren U21 vs Kortrijk U21 | 2.15 | 3.53 | 2.85 |
| 21:30 | 4863 | Maccabi Netanya vs Maccabi Tel Aviv | 5.09 | 3.95 | 1.54 |
| 21:30 | 5171 | St Truiden U21 vs Kmsk Deinze U21 | 1.09 | 8.29 | 16.58 |
| 22:00 | 1992 | RWD Molenbeek U21 vs Westerlo U21 | 2.34 | 3.50 | 2.34 |
| 22:00 | 2057 | Energie Cottbus vs SV Lichtenberg 47 | 1.23 | 5.58 | 9.30 |
| 22:00 | 3210 | Jong PSV vs ADO Den Haag | 2.64 | 3.48 | 2.39 |
| 22:00 | 4130 | Excelsior Virton U21 vs Lommel U21 | 2.19 | 3.65 | 2.43 |
| 22:00 | 4561 | Olympiakos vs Panetolikos | 1.19 | 6.16 | 13.81 |
| 22:00 | 4688 | Rio Ave vs GD Estoril | 2.26 | 3.05 | 3.30 |
| 22:00 | 4893 | Lierse SK U21 vs AS Eupen U21 | 4.99 | 4.16 | 1.52 |
| 22:00 | 5948 | Jong Utrecht vs Telstar | 2.51 | 3.36 | 2.57 |
| 22:30 | 5583 | AC Reggiana vs Gubbio | 1.75 | 3.50 | 4.67 |
| 22:45 | 1886 | Darvel FC vs Falkirk FC | 4.15 | 4.46 | 1.58 |
| 22:45 | 2263 | Sampdoria vs Inter | 7.14 | 4.36 | 1.41 |
| 22:45 | 4033 | Metz vs Caen | 2.21 | 3.16 | 3.21 |
| 23:00 | 1872 | Barracas Central vs Union Santa Fe | 2.64 | 2.85 | 2.70 |
| 23:00 | 2624 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.34 | 3.04 | 2.26 |
| 23:00 | 3607 | Tigres FC (COL) vs Barranquilla FC | 1.73 | 3.31 | 4.55 |
| 23:00 | 3748 | Racing Santander vs Leganes | 2.71 | 2.81 | 2.81 |
| 23:00 | 3906 | Liverpool vs Everton | 1.49 | 4.27 | 5.75 |
| 23:00 | 5422 | FBC Melgar vs Deportivo Municipal | 1.15 | 6.21 | 14.50 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SINGIDA BIG STARS YAPAA NAFASI YA 3 LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa zamani wa timu za Simba na Yanga, Meddie Kagere na Yacouba Songne, jana walifunga mabao kwa timu zao mpya, Singida Big Stars na Ihefu FC, zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali mkoani Mbeya.

Kagere, raia wa Rwanda ambaye aliachwa na Simba mwanzoni mwa msimu huu, alianza kuipatia Singida Big Stars bao dakika ya 63 baada ya kuunganisha kwa kichwa cha kuchupa krosi iliyopigwa pia na mchezaji wa zamani wa timu hiyo raia wa Ghana, Nicolaus Gyan.

**Bao hilo lilidumu kwa dakika tisa tu kabla ya kusawazishwa na Songne raia wa Burkina Faso ambaye aliondoka Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili.**

Mchezaji huyo aliyeingia kipindi cha pili, aliugusa mpira wa faulo iliyopigwa na Samuel Onditi ambao ulimpoteza maboya kipa Benjamin Haule na kujaa ndani ya wavu. Ihefu itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kuondoka na ushindi kwenye mechi ya jana, kwani ilikosa mkwaju wa penalti kabla ya kusawazisha bao hilo.

Kipa Haule alipangua kwa ustadi penalti ya Never Tegere na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Penalti hiyo ilitokana na beki wa zamani wa Simba, Pascal Wawa aliyemwangusha mchezaji mmoja wa Singida Big Stars. Ilikuwa ni mechi ya kwanza kwa Songne, pamoja na Nelson Okwa ambaye anaichezea Ihefu kwa mkopo akitoka Simba.

Kwa matokeo hayo, Singida Big Stars imekwea hadi nafasi ya tatu ikiwa na pointi 44, ikiiengua kwenye nafasi hiyo Azam FC, huku Ihefu ikishika nafasi ya nane kwa kufikisha pointi 27.

# Robertinho aanika

INATOKA UKURASA 24

mechi yake ya Jumamosi dhidi ya vinara wa Kundi C, Raja Casablanca.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, aliwaambia waandishi wetu kuwa baada ya mchezo wa juzi na Horoya AC, jana jioni kikosi kilifanya mazoezi ya utimamu wa mwili kabla ya leo kuanza safari ya kurudi Dar es Salaam, Tanzania.

Alisema Kikosi kitapita Ethiopia na kupumzika kwa muda kabla ya kuendelea na safari ambapo wanatarajia kufika Dar es Salaam kesho (Jumanne) saa 9:00 alfajiri.

"Tutakaporejea Dar es Salaam, wachezaji wataingia kambini moja kwa moja kujiandaa na mchezo dhidi ya Raja Casablanca katika uwanja wetu wa nyumbani, pia kuhusu mshambuliaji wetu, Saido Ntibazonkiza, sasa yuko fiti na tayari kwa ajili ya kuitumikia timu katika mchezo ujao," alisema Ahmed.

Alisema Saido alikuwa na mazoezi maalum pindi timu ilipokuwa Guinea na sasa ataungana na wachezaji wenzake baada ya kupona majeraha.

"Saido tayari amerejea kwenye ubora wake baada ya kupona majeraha yaliyomweka nje siku chache na alikuwa na programu maalum kwa ajili ya kujiweka fiti kwa mechi ijayo dhidi ya Raja Casablanca na Azam FC, atakuwa miongoni mwa kikosi," alisema Ahmed.

Saido aliumia katika mchezo dhidi ya Singida Big Stars baada ya kuchezewa rafu na Hamis Ndemla, ambapo alilazimika kufanyiwa matibabu na kupewa mazoezi maalum wakati kikosi cha timu ya Simba kilipokuwa Guinea.

Tayari Simba imetangaza viingilio vya mchezo huo dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, ambapo cha chini ni Sh. 5,000 eneo la mzunguko, VIP B na C ni Sh. 20,000, VIP A Sh. 30,000 wakati Platinum ni Sh. 100,000 huku Platinum Plus ikiwa ni Sh. 150,000.

Kwa upande wa Platinum atakayenunua tiketi atanufaika na usafiri kutoka Hoteli ya Hyatt Regency mpaka uwanjani na kurudishwa hotelini hapo baada ya mechi huku gari likisindikizwa na polisi.

Lakini kwa mujibu wa Ahmed, watakaonunua tiketi hizo za Platinum watanufaika na kifurushi maalum kutoka Simba, chakula na vinywaji wakiwa uwanjani, ambapo alisema tayari tiketi zimeanza kuuzwa kwa njia ya mtandao na baadaye jana walitarajia kutangaza vituo mbalimbali vitakavyouza.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Hadija Mngwai***




Meddie Kagere

# Michezo

Jumatatu Februari 13, 2023

Nipashe




Arteta alia na bao la Brentford

UKURASA 21

# Robertinho atoa sababu kipigo CAF

## ●●● Aigeukia Raja Casablanca Jumamosi kwa Mkapa, watangaza kuiona buku tano tu huku sasa wakipania...

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema nafasi tatu za wazi walizopoteza wachezaji wake wakiwa ndani ya eneo la hatari ndizo zilizowagharimu juzi nchini Guinea, wakichapwa bao 1-0 dhidi ya Horoya kwenye Uwanja wa Jenerali Lansana Conte jijini Conakry.

**Akizungumza kutoka nchini humo baada ya kumalizika mechi hiyo Robertinho alisema kipindi cha pili waliwakamata kisawasawa wapinzani wao, na kama si wachezaji wake kukosa mabao matatu ya wazi wakiwa ndani ya eneo la hatari, basi wangetoka na ushindi.**

Kwenye mechi hiyo, nahodha John Bocco alishindwa kuweka mpira wavuni akibaki na kipa Moussa Camara mara mbili, huku Clatous Chama naye akikosa bao la wazi baada ya kupiga mpira juu, akiwa ndani ya sita. Pia kipa Aishi Manula aliokoa mkwaju wa penalti kwenye mechi hiyo.

"Kipindi cha kwanza wapinzani wetu walicheza vizuri na wakapata bao moja, na wachezaji wangu walionekana kuwa na uchovu wa kusafiri kwa umbali mrefu, lakini kipindi cha pili nilibadilisha wachezaji wawili ambao walibadilisha mchezo.

"Tumepoteza nafasi tatu za wazi tukiwa ndani ya eneo la hatari, nafikiri nitoe pongezi kwa wachezaji wangu kwa kucheza vema kipindi cha pili na wapinzani kucheza vizuri kipindi cha kwanza," alisema kocha huyo.

Hata hivyo, alisema Horoya pia walipata ushindi huo kwa kunufaika kucheza nyumbani, hivyo nao wanarejea nchini kukutana na mpinzani mwingine ambaye ni Raja Casablaca ya Morocco, ambayo Ijumaa iliyopita iliangushia Vipers ya Uganda kipigo cha mabao 5-0 kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano jijini Casablanca.

"Kwenye mechi hii Horoya walikuwa wanacheza nyumbani na wamenufaika na wenyeji na sisi tunarudi nyumbani. Tunarudi kuangalia mpinzani mwingine tutakayecheza naye kwenye mechi muhimu ambayo sasa nasi tutakuwa nyumbani, tutakuwa mbele ya mashabiki wetu wakitushangilia, kama Raja ni timu kubwa, na Simba nayo ni kubwa vile vile kwa nini tusishinde?" Alihoji kocha huyo.

Bao la wenyeji lilifungwa dakika ya 18 na Pape Abdou N'Diaye akiunganisha kwa kichwa mpira wa kona ambayo mabeki wa Simba walimsahau mchezaji huyo.

Ni matokeo ambayo yaliweka Simba kwenye nafasi ya tatu ya msimamo, huku ikisubiri

HABARI UK.23



MILIKI...


Kiungo wa Simba, Ismael Sawadogo, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Horoya AC, kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Jenerali Lansana Conte jijini Conakry, Guinea juzi na kumalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0. **PICHA: SIMBA**

### Wakali watano usajili wa Januari

**LONDON,** England

DIRISHA la usajili la msimu wa baridi wa 2022/23, lilikuwa la kukumbukwa kwani klabu za Ligi Kuu England, haswa Chelsea, zilitumia fedha nyingi kwa wachezaji wapya. Hata hivyo, si wao pekee walionyakua vichwa vya habari huku klabu...

HABARI UK.11



### Vinara wa penalti Ligi Kuu Bara 2023

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Dodoma Jiji imeweka rekodi ya aina yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kupata penalti...

HABARI UK. 20

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >